SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 3




## Mpango akerwa uchafu Dodoma, atoa agizo zito

# MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*



'BUTTER CHICKEN'
Furahia kuku wa minofu



NYUMBA:
Dondoo za kusafisha bafu na choo katika nyumba yako



KATUNI



MIKONO LAINI
Namna ya kulainisha viganja vyako


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 16, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580827

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Wasichana vinara Kidato cha Nne

**214** wafutiwa matokeo, Hisabati bado mfupa mgumu, aliyeongoza kitaifa aanika siri, ndoto zake... *Endelea ukurasa 2*



Mwanafunzi aliyeongoza kitaifa, Consolata Lubuva

### WATAHINIWA 10 BORA KITAIFA
KIDATO CHA NNE 2021

| | | |
|---|---|---|
| 1. CONSOLATA LUBUVA | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |
| 2. BHUTOI NKANGAZA | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |
| 3. WILIHELMINA MUJARIFU | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |
| 4. GLORY MBELE | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |
| 5. MARY NGOSO | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |
| 6. HOLLY LYIMO | BRIGHT FUTURE GIRLS | DSM |
| 7. BRANDINA CHIWAWA | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |
| 8. IMAM MOGAEKA | FEZA BOYS | DSM |
| 9. MFAUME MADILI | ILBORU | ARUSHA |
| 10. CLARA ASSENGA | ST. FRANCIS GIRLS | MBEYA |

### SHULE 10 BORA KITAIFA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | KEMEBOS | (KAGERA) |
| 2. | ST. FRANCIS | (MBEYA) |
| 3. | WAJA BOYS | (GEITA) |
| 4. | BRIGHT FUTER GIRLS | (DAR) |
| 5. | BETHEL SABS GIRLS | (IRINGA) |
| 6. | MAUA SEMINARY | (K/NJARO) |
| 7. | FEZA BOYS | (DAR) |
| 8. | PRECIOUS BLOOD | (PWANI) |
| 9. | FEZA GIRLS | (DAR) |
| 10. | MZUMBE | (MORO) |



Kaimu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Taifa, Dorothy Semu

## ACT yatoa mapendekezo saba tume huru uchaguzi

UKURASA 3

## Wanachama wanaowania Uspika CCM wafikia 71

UKURASA 4

MICHEZO YANGA YAPANIA KUVUNJA MWIKO UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

## Wafutiwa matokeo kisa udanganyifu

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Taifa la Mitihani (NECTA) limewafutia matokeo watahiniwa 214 katika mitihani ya darasa la nne, kidato cha pili na kidato cha nne kwa hutuma za kufanya udanganyifu.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu taarifa ya matokeo ya darasa la nne, kidato cha pili na kidato cha nne kwa mwaka 2021.

Kwenye taarifa yake hiyo, Dk. Msonde alisema kati ya watahiniwa waliobainika kufanya udanganyifu, watahiniwa 83 ni wa darasa la nne, watahiniwa 27 ni kidato cha pili, wengine 102 ni kidato cha nne na wawili ni wa mtihani wa maarifa (QT).

Dk. Msonde alisema: "Baraza la Mitihani limefuta matokeo yote ya watahiniwa 214 waliofanya udanganyifu katika mtihani kwa mujibu wa kifungu cha 5(2)(i) na (j) cha Sheria ya Baraza la Mitihani Sura ya 107 kikisomwa pamoja na cha 30(2)(b) cha Kanuni za mitihani.

Kadhalika, Dk. Msonde alisema pia NACTE limezuia kutoa matokeo ya watahiniwa 555 ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo.

Alieleza kuwa watahiniwa hao wamepewa fursa ya kufanya mtihani kwa masomo ambayo hawakufanya kwa sababu ya ugonjwa kwa mwaka 2022 kwa mujibu wa kifungu vha 32(1) cha kanuni za mitihani.



Wanafunzi wa shule ya Feza, Loi Kitundu wa kidato cha pili (kushoto) na Imam Mogaeka wa kidato cha nne, wakipongezwa na walimu wao, shuleni hapo, jijini Dar es Salaam jana, baada ya Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kutangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha nne na cha pili, ambapo shule hiyo imeingia katika kumi bora huku wanafunzi hao wakishika nafasi ya saba kitaifa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wasichana vinara kidato cha nne

**Na Mary Geofrey**

Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), limetangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2021 huku ikionyesha ufaulu umeongezeka, wanafunzi wa kike waking'ara kulinganisha na wa kiume.

Akitangaza matokeo hayo jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alisema watahiniwa 483,820 sawa na asilimia 87.30 wamefaulu mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2021.

Dk. Msonde alisema kati ya watahiniwa 483,820 wasichana waliofaulu ni 218,174 sawa na asilimia 85.77, huku wavulana wakiwa 204,214 sawa na asilimia 89.

"Mwaka 2020 watahiniwa 373,958 sawa na asilimia 85.84 wa shule walifaulu mtihani huu. Hivyo ufaulu wa watahiniwa wa shule umeongezeka kwa asilimia 1.46 ikilinganishwa na mwaka 2020," alisema Dk.Msonde.

Katika matokeo hayo yalionyesha wasichana wanane kati ya 10 wameingia kwenye orodha ya wanafunzi 10 bora waliofanya vizuri kwenye matokeo ya mtihani wa kidato cha nne uliofanyika Novemba, mwaka jana.

Kati ya hao, wasichana saba wanatoka Shule ya St. Francis Girls, iliyoko mkoani Mbeya, msichana mwingine akitoka Shule ya Bright Future Girls ya Dar es Salaam , huku wavulana wawili pekee waliongia kwenye 10 bora kitaifa wakitoka shule za Feza Boys ya Dar es Salaam na Ilboru ya Arusha.

Walioingia kwenye orodha hiyo ni pamoja na Consolata Lubuva, Buthoi Nkangaza, Wilihelmina Mujarifu, Glory Mbele na Mary Ngoso, wote kutoka shule ya St. Francis Girls.

Wengine ni Holly Lyimo (Bright Future Girls), Blandina Chiwawa (St. Francis Girls), Imam Mogaeka (Feza Boys), Mfaume Madili (Ilboru) na Clara Assenga (St. Francis Girls).

Dk. Msonde alizitaja shule 10 bora zilizofanya vizuri kitaifa kuwa ni Kemebos (Kagera), St. Francis Girls (Mbeya), Waja Boys (Geita), Bright Future Girls (Dar es Salaam) na Bethel Sabs Girls (Iringa).

Zingine ni Maua Seminary (Kilimanjaro), Feza Boys (Dar es Salaam), Precious Blood (Pwani), Feza Girls (Dar) na Mzumbe (Morogoro).

**WAVULANA JUU MADARAJA**

Pamoja na kwamba wasichana wameng'ara katika wanafunzi 10 bora kitaifa, matokeo yanaonyesha kuwa wavulana wamewashinda wasichana katika viwango vya madaraja. Kwa daraja la kwanza, wavulana waliofaulu kiwango hicho ni 19,152 (asilimia 8.35) wakati wasichana ni 12,623 (asilimia 4.96). Kwa daraja la pili, wavulana ni 34,856 (asilimia 15.19) na wasichana ni 25,419 (asilimia 9.99).

Waliofaulu katika daraja la tatu, wasichana ni 44,357 (asilimia (19.33) na wasichana ni 37,014 (asilimia 14.55). Waliopata daraja la nne wavulana ni 105,848 (asilimia 46.13) na wasichana 143.,118 ambao ni asilimia 56.26.

Kwa matokeo ya jumla, waliopata ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu, wavulana ni 98,388 sawa na asilimia 42.87 na wasichana 75,056 ambao ni asilimia 29.51. kwa matokeo ya daraja la kwanza hadi la nne, wavulana ni 204,214 (asilimia 89) na wasichana 218,174 sawa na asilimia 85.77.

Katika kundi la waliofeli, wavulana ni 25,231 sawa na asilimia 11 na wasichana ni 36,201 ambao ni asilimia 14.24 ya watahiniwa katika makundi yao.

**HISABATI SHIDA**

Licha ya matokeo ya mwaka 2021 kuonyesha kuwa ufaulu umepanda kulinganisha na 2020, somo la Hisabati limeonekana kuwa bado mfupa mgumu kwa watahiniwa kutokana na ufaulu wake kuwa wastani wa asilimia 19.54.

Wakati somo hilo likionekana kikwazo, masomo ya Kiswahili na Kemia ndiyo ambayo wanafunzi wamefanya vizuri kwa wastani mzuri ikilinganishwa na masomo mengine na wastani wa ufaulu wa asilimia 956.99 na 92.02 mtawalia.

# Aliyeongoza kitaifa aanika siri mafanikio

**Na Waandishi Wetu**

MTAHINIWA wa kidato cha nne kutoka Shule ya Sekondari St. Francis Girls, Consolata Lubuva, aliyeongoza kitaifa kwenye matokeo ya kitaifa mwaka 2021, ametaja siri ya mafanikio yake pamoja na ndoto yake.

Akizungumza na Nipashe nyumbani kwao Salasala mkoani Dar es Salaam, Consolata alisema amepokea kwa furaha matokeo hayo kwa kuwa matarajio yake yalikuwa ya wastani lakini amefanya viruzi.

"Siri ya mafanikio haya ni Mungu. Nilikabidhi masomo haya kwa Mungu naye amenisaidia. Wazazi wamekuwa msaada mkubwa kwangu pia wamekuwa mfano mzuri sana. Mfano mama yangu ni daktari wa falsafa amenihamasisha sana," alisema Consolata na kuongeza;

"Pia nilijitahidi kupanga muda wangu vizuri, nilihakikisha nina muda wa kusoma, kusali na kufanya mambo muhimu ya shule. Haya ndiyo yalinipa mafanikio."

Alisema ataongeza juhudi zaidi ili afikie ndoto yake ya kuwa daktari wa watoto.

Consolata alitaja mambo yaliyomwezesha kuongoza katika mtihani huo ni kusoma kwa bidii na kufanya maombi na kwamba wakati matokeo hayo yanatangazwa, alikuwa akisikiliza nyimbo za injili nyumbani kwao, Salasala.

"Nilikuwa natarajia kuwa naweza kuingia kwenye kumi bora kitaifa lakini si kuongoza kwa kuwa namba moja," alisema Consolata.

Alisema wakati akifanya mtihani, somo pekee lililomsumbua ni Fizikia, lakini mengine hayakuwa tatizo kiasi cha kumpa ujasiri kuwa angefaulu mitihani yake ya kidato cha nne.

**VINARA WENGINE**

Nipashe ilifika katika Shule ya Sekondari St. Francis na kukutana baadhi ya wanafunzi waliofanya vizuri akiwemo Bhutoi Nkangaza aliyeshika nafasi ya pili kitaifa na Glory Mbele ambaye ameshika nafasi ya nne. Wanafunzi hao walitaja sababu mbalimbali zilizowafanya wang'are kwenye matokeo hayo kitaifa na kuifanya shule yao ishike nafasi ya pili kitaifa. Bhutoi alisema wakati matokeo yanatangazwa alikuwa yupo nyumbani kwao na alikuwa hana taarifa yoyote na alipigiwa simu na wenzake lakini bado hakuamini.

Alisema alipofika nje alimkuta mama yake akiwa analia kwa furaha na ndipo akaamini kuwa alichoambiwa na wenzake ni kweli na kwamba alianza kupokea simu nyingi za kumpongeza.

Siri ya mafanikio yake, alisema ni kusoma kwa bidii, kumuomba Mungu pamoja na ushirikiano mzuri baina ya wanafunzi hao akidai kuwa walikuwa wanasaidiana kwenye maeneo ambayo walikuwa wanaamini kuwa ni magumu.

Hata hivyo Bhutoi ambaye ana ndoto ya kuwa daktari wa watoto aliwataka wanafunzi wengine waliobaki shuleni hapo kusoma kwa bidii ili na wao wafikie mafanikio waliyoyafikia wao, huku akiwashukuru walimu na wazazi kwa kuwasaidia.

Naye Glory ambaye ameshika nafasi ya nne kitaifa alisema mazingira ya shule yao yanavutia wanafunzi hao kusoma kwa bidii na kwamba pia walimu wa shule hiyo wanawafundisha kujitambua kuanzia hatua za mwanzo wanapojiunga kidato cha kwanza.

**Imeandaliwa na Mary Geofrey, Salome Kitomari (Dar) Nerbart Msokwa (Mbeya).**

HABARI KITAIFA

## Utafiti kufanywa kuongeza watalii

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema wizara hiyo inatarajia kufanya utafiti kuhusu utalii wa ndani na mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa.

Akizungumza jana Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa utafiti huo unaoratibiwa na Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Dk. Ndumbaro alisema utafiti huo pia utasaidia kujua sera, sheria, kanuni na miongozo katika kuboresha sekta hiyo.

Utafiti huo, alisema utasaidia katika kutekeleza dira ya maendeleo ya miaka mitano, kupanua wigo wa kupokea watalii wa ndani na nje, kitendo kitakacholeta chachu katika ukuaji wa sekta ya utalii nchini.

"Katika utafiti huu tumeona tukitumie Chuo Kikuu Huria kwani kina wataalamu wa kutosha, hivyo kwa muda wa miezi minne iliyotolewa, tunatarajia watatupatia matokeo mazuri na kwa wakati," alisema Ndumbaro.

Kwa mwaka 2021 alisema idadi ya watalii wa ndani ilifikia 700,000, huku watalii wa nje wakiwa 900,000. Alisema idadi hiyo ni kubwa na haijawahi kutokea.

Pia alisema ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inawataka ifikapo mwaka 2025 mapato yanayotokana na utalii yafikie Sh. bilioni sita na idadi ya watalii ifike milioni 25. Dk. Ndumbaro alisema fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa utafiti huo zitasaidia kutimiza malengo hayo.

"Matumizi ya fedha yawe mazuri pasipo kuleta chenga chenga kwani fedha hizo zingeweza kutumika sehemu nyingine ila Rais akaona aziingize huku ili kusaidia kuleta maendeleo katika sekta hii, hivyo zitumike vizuri ili tufikie malengo," alisema Ndumbaro.

Mshauri Elekezi kutoka OUT, Prof. Ladislaus Batinoluho, alisema katika utafiti huo wanatarajia kufikia watu katika zaidi ya kaya 33800 watakaowatumia katika kukusanya taarifa kwa ajili ya kupima ukubwa wa utalii nchini.

Pia alisema utafiti huo utasaidia kukadiria idadi ya watalii wa ndani na nje, huku akieleza kuwa katika utekelezaji wa kukusanya taarifa hizo watawapatia mafunzo zaidi wataalamu 31 ambao watawasaidia katika ukamilishaji wa suala hilo.

"Chuo Kikuu Huria kina matawi kila sehemu nchini, hivyo wakusanya taarifa 676 watatumika na utafiti huu utaendeshwa kwa muda wa miezi minne na takwimu zitakazotokana na utafiti huu zitasaidia kuonyesha mwelekeo na kutoa ushauri mbalimbali utakaochochea maendeleo katika sekta ya utalii nchini"

# ACT- Wazalendo yatoa mapendekezo saba kuundwa tume huru ya uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT - Wazalendo kimesema kinaanza na hoja ya Tume Huru ya Uchaguzi ili kuweka mazingira ya kupata Katiba Mpya inayotokana na maoni na matakwa ya wananchi.

Kaimu Mwenyekiti wa chama hicho, Dorothy Semu, amesema mwaka huu utakuwa wa kuipigania tume hiyo ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa taifa.

Semu aliyasema hayo jana kwenye taarifa iliyotolewa na chama hicho, baada ya kikao cha viongozi wa ACT- Wazalendo wa Majimbo yote ya Mkoa wa Arusha.

"Msimamo wa ACT-Wazalendo upo bayana. Tunaanza na Tume Huru ya Uchaguzi ili kuweka mazingira ya kupata Katiba Mpya inayotokana na maoni na matakwa ya Wananchi.

"Sababu za kuhitaji tume kwanza ziko wazi. Tunataka mchakato wa kura ya maoni ya Katiba Mpya usimamiwe na tume ambayo ni huru. Pia kwa kuzingatia ukweli kuwa mchakato wa kupatikana kwa Katiba Mpya na kuanza kutumika, unaweza kuhitaji muda zaidi, tunataka uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu 2025 usimamiwe na tume huru ya uchaguzi". Alisema.

Kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa tume hiyo, Semu alisema ACT-Wazalendo inapendekeza Sheria Mpya ya Uchaguzi 2022, iweke utaratibu kuwa Watanzania wanaotaka kuwa wajumbe wa tume huru ya uchaguzi waombe kazi kwa tangazo la wazi kwa umma.

Pia alisema sheria hiyo ianzishe kamati maalumu ya uteuzi wa mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa tume huru ya uchaguzi huku akibainisha kuwa kamati ya uteuzi ifanye usaili, iwe na uwazi kwa waombaji wote na kuchuja majina ambayo yatapelekwa kwa rais kwa ajili ya uteuzi.

"Baada ya wajumbe wa tume huru ya uchaguzi kupatikana, wataajiri mkurugenzi wa uchaguzi ambaye nafasi itatangazwa, kufanyiwa usaili wa wazi na kisha jina kupelekwa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi," alisema.

Semu alibaisha kamati ya uteuzi wa tume itamkwe kisheria kuongozwa na Jaji Mkuu wa Tanzania kama Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Zanzibar kama Makamu wa Mwenyekiti, Wajumbe wawe Rais wa Tanganyika Law Society, Rais wa Zanzibar Law Society, mtu mmoja atakayeteuliwa na mkuu wa shughuli za serikali bungeni, na atakayeteuliwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kama hakuna Kambi rasmi ya upinzani bungeni, basi kutoka chombo kinachojumuisha vyama vyenye wabunge bungeni.

Semu alisema pia mtu mmoja atatoka asasi ya kitaifa ya masuala ya sheria na haki za binadamu Tanzania bara na mwingine kutoka asasi kama hiyo Tanzania Zanzibar. "Kwa vyovyote vile angalau theluthi ya wajumbe wa kamati ya uteuzi lazima wawe wanawake. Kutakuwa na sifa maalumu za mwenyekiti na wajumbe wa tume huru ya uchaguzi ili kuhakikisha wanakuwa watu wenye weledi na hawaegemei upande wowote," alibainisha.

Kuhusu mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya, Semu alisema ACT Wazalendo inapendekeza bunge kuunda kamati ya wataalamu ili kutafuta namna bora ya kumalizia mchakato huo kwa sababu Katiba Pendekezwa haikutokana na maridhiano ya pande zote baada ya wapinzani kususia hatua ya kupiga kura katika Bunge la Katiba.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akiangalia lundo la takataka zilizotelekezwa nje ya soko kuu la Majengo, jijini Dodoma jana, alipofanya ziara ya kushtukiza kukagua hali ya usafi katika eneo hilo, ambapo alitoa muda wa wiki mbili ziwe zimetolewa. **PICHA: OMR**

# Mpango akerwa taka jiji la Dodoma

**Na Paul Mabeja**,DODOMA

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, ameeleza kukerwa na taka katika jiji la Dodoma na kutoa wiki mbili kwa uongozi wa jiji hilo kuondoa taka zote zilizozagaa mitaani.

Sambamba na hilo, amemwagiza Mkurugenzi wa Jiji hilo kuvunja mkataba na Kampuni ya Usafi wa Mazingira ya Green Waste.

Alitoa maagizo hayo baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kukagua usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya Soko la Majengo na kubaini kuwapo kwa mlundikano wa taka nyingi.

Dk. Mpango alisema ni aibu kwa Jiji la Dodoma ambalo ndilo makao makuu ya nchi kuwa na mlundikano wa uchafu katika maeneo ya masoko ambayo yanatumiwa na watu kufanya biashara mbalimbali za vyakula.

Pia aliwaagiza wakurugenzi wa majiji yote nchini kuhakikisha suala la usafi linapewa kipaumbele na kuwa endelevu.

"Jiji la Dodoma ni chafu sana mnashindwa hata na Dar es Salaam. Wao wako vizuri na kule ndiko kuna fujo sana. Kwa mfano barabara hii ya kutoka Arusha pembezoni kumejaa taka. Sasa ndani ya wiki mbili nataka nzuri nakaa hapa Dodoma lazima nitakuja kukagua,"alisisitiza Dk. Mpango. Kuhusu kampuni ya usafi ya Green Waste alimtaka Mkurugenzi wa Jiji kuvunja mkataba na kampuni hiyo baada ya kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema moja ya changamoto wanayokabiliana nayo ni uhaba wa magari kwa ajili ya kuzoa taka hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alisema atahakikisha kuwa maagizo ya Makamu wa Rais yanafanyiwa kazi.

"Tutahakikisha kuwa tunatekeleza maagizo yote katika muda uliotupatia na leo hii viongozi wote wa jiji na wilaya watabaki hapa kufanya vikao ili kupata suluhu ya kuziondoa taka hizi," alisema Mtaka.

HABARI KITAIFA

# Wanaowania Uspika CCM wafikia 71

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JANA ikiwa ni siku ya mwisho ya uchukuaji na urudishaji fomu ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kuwania uteuzi wa nafasi ya Spika wa Bunge, wanachama 71 ndio waliojitokeza kuwania kinyang'anyiro hicho. Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Katibu Msaidizi Mkuu Idara ya Oganaizesheni CCM, Solomon Itunda, alisema wanachama waliochukua fomu hadi pazia linafungwa ni 71.

Alisema kwa siku ya jana wanachama watano walichukua fomu na kufunga idadi hiyo ya wanachama waliojitokeza kuomba nafasi hiyo.

"Leo (jana) hii tumepokea wanachama watano ambao wamejitokeza katika vituo vyetu vya Dodoma na Dar es Salaam kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa kugombea nafasi hii ya Uspika iliyoachwa wazi," alisema Itunda.

Itunda alisema kwa siku ya jana katika kituo cha Dodoma ni mwanachama mmoja ndiye aliyejitokeza kuchukua fomu wakati katika Ofisi ya Lumumba jijini Dar es Salaam ni wanachama wanne na Afisi Kuu ya Zanzibar hakuna mwanachama aliyejitokeza kuchukua.

Itunda, alimtaja aliyechukua fomu Ofisi Kuu ya CCM Dodoma kuwa ni Samwel Magero.

"Ofisi ndogo ya Lumumba waliochukua fomu ni Rahimuddin Ismail, Alex Mwita, Themistocles Laurian Rwegasira pamoja na Grangay Nyalohala," alisema Itunda.

Alisema kukamilika kwa kazi hiyo ya kuchukua fomu iliyoanza Januari 10, mwaka huu kunatoa nafasi kwa vikao vingine kuanza.

"Baada ya kuchukua na kurejesha fomu, sasa hatua inayofuata ni vikao vingine kuketi ili kuanza kufanya mchujo wa kupitisha jina moja litakalo kiwakilisha chama katika kugombania nafasi hii ya Uspika," alisema Itunda.

Alisema pamoja na wanachama hao 71 kuchukua fomu lakini kati yao wawili wameshindwa kurejesha.

Aidha, alitoa shukrani kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha demokrasia ndani ya chama hicho.

"Lakini pia ninawashukuru wanachama wote ambao wamejitokeza kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa na chama," alisema.


A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422


# CWT yampongeza Rais ujenzi madarasa

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Morogoro kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika mikoa yote nchini.

Kimesema hatua hiyo itasaidia kupungunza msongamano wa wanafunzi madarasani na kurahisisha ufundishaji kwa walimu.

Pongezi hizo zilitolewa jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Morogoro, Jumanne Nyakirangani, wakati akizungumza kuhusu manufaa yatakayopatikana kutokana na ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa nchini.

Alisema uwapo wa vyumba hivyo vya madarasa hasa katika Mkoa wa Morogoro utasaidia pia walimu kuwa na mazingira mazuri ya ufundishaji, utulivu kwa wanafunzi.

"Ni wazi kuwa utulivu utapatikana kwa wanafunzi kwani zamani unakuta darasa moja lilikuwa na wanafunzi zaidi ya 150 ambayo ilikuwa inapoteza utulivu kwa walimu, kwahiyo vyumba hivi vitasaidia walimu kufundisha wakiwa na amani," alisema Nyakirangani.

Aidha, aliwaomba wazazi kujitokeza kwa wingi kuwaandikisha watoto ili waweze kupata elimu bora itakayowafaa katika maisha yao ya baadaye.

"Niwaombe wazazi jitokezeni kwa wingi kuwapeleka watoto shule, mazingira yaliyoandaliwa na Rais Samia ni mazuri mnoo, hivyo msirudi nyuma endeleeni kuiunga mkono Serikali kwa kupeleka watoto shule," alisema.

Aidha, alimpongeza Rais Samia kwa kusikiliza madai ya walimu ya kupandishwa madaraja na maslahi mengineyo ambayo wameahidiwa kuwa yatafanyiwa kazi kwa wakati.

Nyakirangani alisema: "Mwaka jana zaidi ya watumishi 100,000 walipandishwa vyeo, wengi wao walikuwa ni walimu, pia walimu wanaendelea kupandishwa madaraja na viongozi wameshapatiwa mafunzo na sasa tunakwenda kutoa hayo mafunzo kwa wanachama".

# Waziri Mhagama awataka maofisa utumishi kujipanga

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amewataka watumishi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu serikalini kujipanga kiutendaji, ili kuhakikisha wananchi wanaohudumiwa wanafurahia huduma zinazotolewa.

Alitoa wito huo jana jijini Dodoma, wakati wa kikao kazi kati yake na watumishi wa Idara ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini, chenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa idara hiyo.

Jenista alisema anataka ufike wakati mtumishi wa umma anayedai haki ambayo amedhulumiwa kwa muda mrefu na mwajiri wake pindi akisikia kuwa suala lake limewasilishwa Ofisi ya Rais-Utumishi afurahi na kuwa na matumaini kuwa litafanyiwa kazi kwa wakati.

"Nataka mtumishi wa umma aliyekata tamaa ya kutolipwa malimbikizo yake ya mishahara au kupewa stahiki zake nyingine akisikia suala lake limewasilishwa kwetu afurahi na kuamini kuwa suala lake litafanyiwa kazi kwa haki na wakati," alisema Jenista.

Alisema idara hiyo ikifanya kazi kwa uadilifu na weledi itakuwa imetoa mchango mkubwa katika kujenga morali ya utendaji kazi wa watumishi wa umma nchini, ikiwa ni pamoja na kujenga imani ya wananchi kwa serikali yao.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi na watumishi wa umma kuutumia vema mfumo wa 'Sema na Waziri wa Utumishi' (www.swu.go.tz) kuwasilisha changamoto na malalamiko ya masuala ya kiutumishi na utawala bora, ili yaweze kufanyiwa kazi.

"Mimi waziri mwenye dhamana ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kusimamia masuala ya kiutumishi na utawala bora napenda nipokee changamoto zinazowakabili watumishi wa umma kupitia mfumo huu hivyo, watumishi muutumie ipasavyo," alisema Jenista.


KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU FAIDHA RASHID ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 909 BHT** aina ya **BOXER 150** Rangi Nyekundu yenye Chasis No. ***MD2A21BZ7GWB89606*,** Engine No. **PFZWGB03930.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **DOD/TR/RB/470490/2021**

116653702

# HABARI KITAIFA

## RC ataka viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIONGOZI wa madhehebu ya dini nchini wametakiwa kuliombea taifa liendelee kuwa na amani kwa sababu sasa hivi linapitia katika kipindi kigumu cha maadui wengi ambao wanataka kuvuruga amani.

Ombi hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, wakati akitoa hotuba kwenye hitimisho la siku 10 za maombi katika Kanisa la Wadventista Wasabato lililopo Shinyanga Mjini.

Mkude ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema kipindi hiki viongozi wa dini wanapaswa kuongeza maombi ya kuliombea Taifa, pamoja na kumuombea Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali yote, ili wafanye kazi vizuri ya kuwatumikia wananchi.

"Nalipongeza sana Kanisa la Waadventista Wasabato Shinyanga Mjini kwa kufanya maombi ya kuliombea Taifa liendelee kuwa na amani na Rais wetu Samia, jambo ambalo ni jema kwa sababu bila Mungu Serikali haiwezi kusonga mbele kuwatumikia wananchi," alisema Mkude

"Nawaomba viongozi wa dini muendelee kuliombea Taifa ambalo kwa sasa linapita kwenye kipindi kigumu cha maadui, ambao wapo kwa ajili ya kutaka kuvuruga amani iliyopo" aliongeza

Kadhalika alisema wananchi wa Mkoa wa Shinyanga wanapaswa kuwapeleka watoto wao shule kwa sababu serikali imeondoa gharama ambayo wanapaswa kulipa.

Aidha, Mkude alilipongeza kanisa hilo kwa kujali watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo watoto na kuwapatia misaada mbalimbali, jambo ambalo amebainisha ni kujipatia baraka.

Akisoma risala kwa niaba ya mchungaji wa kanisa hilo, Lazaro Mbogo, Rafael Lyochi, alisema wameendesha maombi hayo ya siku 10 kwa kuliombea Taifa pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan.

Lyochi alisema katika maombi hayo walijikita kuliombea Taifa liendelee kuwa na amani, ukuaji wa uchumi wa nchi, mvua kunyesha ili wananchi walime na kupata chakula.




Ofisa Kitengo cha Kadi Benki ya NMB, Mary Mwasikili (kulia), akizungumza na mmoja wa wateja walioshinda katika droo ya pili ya Kampeni ya 'NMB Masta Bata Kivyako Vyako', Jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Meneja Kitengo cha Kadi wa Benki hiyo, Sophia Mwamwitwa na Ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Pendo Mfuru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Majaliwa awapa kibarua wataalamu kilimo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema kabla ya kuanza kwa uzalishaji wa mbolea katika kiwanda cha Itracom jijini Dodoma, wataalamu wa Wizara ya Kilimo wanatakiwa kujiridhisha kama mbolea hiyo inaendana na udogo katika maeneo mbambali nchini.

Majaliwa, alisema hayo jana alipofanya ziara kukagua ujenzi wa kiwanda cha mbolea kinachojengwa na mwekezaji kutoka Burundi, eneo la Nala.

Alisema mahitaji ya mbolea nchini ni takribani tani 700,000, hivyo kukamilika kwa kiwanda hicho, kutakua mkombozi kwa wakulima na kuipunguzia serikali mzigo wa kuagiza mbolea nje ya nchi.

"Wizara ya Kilimo pamoja na wataalamu wa mwekezaji, hakikisheni kiwanda hiki kabla ya kuanza uzalishaji, mnafanya utafiti wa aina ya udongo wetu kama unaendana na mbolea hii kabla kuanza kuzalisha," alisema Majaliwa.

Alisema hali hiyo itasadia kuondoa mkanganyiko ambao unaweza kujitokeza baadaye wakati wa uzalishaji mbolea itakapobainika kuwa haiendani na udogo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Nalisema hili kwa kuwa hili lilishawahi kujitokeza katika kiwanda kile cha Minjingu. Kumekuwapo na mijadala mingi kuwa mbolea ile haiendani na udongo wetu. Mijadala hii imekuja hadi Bungeni.

"Lakini wataalamu wetu mpo na mnafanya utafiti kwa nini msimshauri yule mwekezaji ili kiwanda kile kifanye uzalishaji? Nataka kila uwekezaji uliofanyika nchini uwe na maana tena kiwanda kile kingetusaidia kuongeza tani 100,000 ya mbolea," alisema.

Majaliwa pia alisema lengo la serikali ni kuongeza tija katika kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

"Tunataka kupitia kilimo kuwa nchi ambayo itazalisha kwa wingi na kuuza katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashari, nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na bara la Afrika kwa ujumla," alisema Majaliwa.

Pia aliwaagiza viongozi wa serikali, wakiwamo wa mkoa wa Dodoma kuboresha miundombinu ya barabara, umeme na maji ili kukiwezesha kiwanda kuendesha shughuli zake.

"Hatuwezi kuacha uwekezaji mkubwa wa kiwanda kama hichi ambacho kina uwezo wa kuzalisha tani 600,000 za mbolea kwa mwaka ukwame kutokana tu na kukosekana kwa huduma ya maji," alisisitiza

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema mbolea imepanda kwa kasi katika soko la dunia, hivyo ujenzi wa kiwanda hicho utaondoa kero ya upatikanaji wa bidhaa hiyo nchini.

Alisema serikali imekuwa ikitumia takribani Dola za kimarekani milioni 450 kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa mbolea nje ya nchi, fedha ambazo zingetumika kutekeleza miradi mingine ya maendeleo.

## Tanzania yawezeshwa bil. 2.3/- ICAO Kudhibiti, kuimarisha usafiri wa anga

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepokea msaada wa dola milioni moja (takribani Sh. bilioni 2.3) kutoka serikali ya China kupitia Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kusimamia na kudhibiti usafiri wa anga.

Msaada huo unatarajiwa kuchochea ongezeko la ndege za mashirika mbalimbali duniani kutua na kuruka nchini.

Fedha hizo ni matokeo ya ukaguzi mbalimbali ambao umekuwa ukifanywa na ICAO kwa nchi zote zinazotoa huduma za usafiri wa anga, Tanzania ikiwamo, ili kuhakikisha kuna usalama wakati wote.

Akizungumza juzi katika hafla maalumu ya uzinduzi wa mradi huo jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema fedha hizo zitatumika kuboresha miundombinu ambayo kwa sasa inafanyika sambamba na maboresho yanayofanywa na serikali katika Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

"Nawapongeza sana Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya mpaka kuwa miongoni mwa nchi chache ambazo zimepata fedha hizo. Ni imani yangu kuwa hatuturudi nyuma hasa ukizingatia serikali inaboresha shirika letu la ndege," alisema.

Naibu Waziri huyo alitaka TCCIA kuhakikisha fedha zinasimamiwa vizuri ili kuleta tija na matokeo stahiki na hatimaye kubaki kwenye viwango vya juu vya usimamizi na udhibiti wa usafiri wa anga nchini.

Naye Mkurugenzi wa ICAO Kanda ya Afrika Mashariki na Kati, Barry Kashambo, alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, kwa jitihada mbalimbali ambazo amekuwa akizifanya.

Alisema ndani ya miaka miwili ameipandishia TCAA asilimia za usalama na udhibiti kutoka 50 na kufikia 67 na kufanikiwa kupata mkopo kutoka katika shirika hilo.

Mshauri wa Waziri kutoka Ubalozi wa China, Xu Chen, alisema serikali ya China itaendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika sekta mbalimbali ili kuchochea maendeleo ya taifa.

Awali, akitoa taarifa, Johari alisema fedha hizo zitaekelezwa kwenye mafunzo ya wataalamu katika eneo la usalama na ununuzi wa vifaa mbalimbali ili kuimarisha udhibiti na kuongeza usalama katika usafiri wa anga.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## CCM, wabunge wake wateue Spika mahiri

**HATIMAYE** jana dirisha la kuchukua na kurejesha fomu katika kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), lilifungwa rasmi huku wanachama waliojitokeza kuomba nafasi hiyo wakiwa wamefikia 71.

Kwa idadi ya wanachama waliojitokeza, hiyo ni rekodi ambayo haijawahi kutokea katika siasa za Tanzania kuwania nafasi yoyote ile ya kitaifa hasa zile zinazopatikana kwa mchakato wa kuomba, kupendekezwa, kuteuliwa na chama na hatimaye kuchaguliwa katika ngazi husika.

Uchaguzi wa Spika wa Bunge unatarajiwa kufanyika kutokana na aliyekuwa akishika wadhifa huo, Job Ndugai, kujiuzulu baada ya kupata shinikizo kutoka kwa watu mbalimbali kutokana na kauli zake ambazo zilionyesha dhahiri kukinzana na mambo yanayofanywa na serikali yake ya CCM.

Wanachama hao wanawania kuteuliwa na chama na hatimaye kupigiwa kura na wabunge wa CCM ili kumpata mmoja wao atakayegombea nafasi hiyo, kupambana na wagombea wa vyama vingine.

Licha ya kwamba kutakuwa na mchuano katika kinyang'anyiro hicho, ukweli unabaki kwamba mwanachama atakayechaguliwa na Wabunge wa CCM ndiye atakayekuwa Spika wa Bunge. Hiyo inatokana na ukweli kwamba ndani ya Bunge, CCM ina wabunge wengi, hivyo mgombea wao atashinda kwa urahisi kama ambavyo imekuwa ikitokea katika uchaguzi mwingine wowote uliopita wakati wa siasa za vyama vingi.

Kwa ujumla, mchuano wa kumpata mrithi wa Ndugai unaonekana kuwa mgumu kwenye ngazi za uteuzi kwa maana ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) na Kamati Kuu. Wajumbe wa kamati hizo pamoja na ile ya maadili ya CCM, zinatarajiwa kuwa na kazi ngumu kufanya mchujo na kuwapata wanachama watatu watakaopelekwa katika kamati ya wabunge ili kutoa jina moja.

Kazi hiyo inatarajiwa kuwa na ugumu kutokana na baadhi ya wanachama waliojitokeza kuwa mashuhuri na wamewahi kushika nyadhifa kubwa ndani ya serikali pamoja na Bunge lenyewe.

Miongoni mwa watu hao ni Andrew Chenge ambaye miongoni mwa nyadhifa alizoshika ni Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Miundombinu (sasa Ujenzi na Uchukuzi), Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa zaidi ya miaka 10 na mmoja wa wenyeviti wa Bunge. Mwingine ni Dk. Thomas Kashilillah ambaye amewahi kuwa Katibu wa Bunge na Naibu Spika wa sasa, Dk. Tulia Ackson.


Mbali na vigogo hao, pia wamo waliowahi kuwa mawaziri katika serikali wakiwamo Stephen Masele ambaye aliwahi pia kuwa Makamu wa Rais na Kaimu Rais wa Bunge la Afrika (PAP), Dk. Titus Kamani, Sophia Simba, Mussa Azan Zungu na Stella Manyanya.

Pamoja na kuwamo kwa watu maarufu ambao wamechukua fomu, ni dhahiri kwamba kila mwanachama ana sifa zake na CCM itatumia vigezo ilivyojiwekea vikiwamo vya uwezo, uzoefu na uadilifu ili kuwapata wale watakaoonekana wanafaa kushika wadhifa huo.

Watanzania wanachotaka ni Spika bora atakayeliendesha bunge kwa weledi kama baadhi ya waliowahi kushika nafasi hiyo walivyofanya. Pia ni wazi kwamba chama hicho kikongwe katika siasa za Tanzania na Afrika kwa ujumla, kitakuwa kimejifunza vya kutosha kuhakikisha kinateua watu wazuri ili kulinda heshima yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge

## Kampeni za vitamini ya foliki asidi zilete matokeo chanya



Na Sabato Kasika

**JANUARI** 3 hadi 9, mwaka huu, ilikuwa wiki ya kampeni maalumu ya kuhamasisha matumizi ya vitamini ya foliki ili kusaidia jamii kukabiliana na tatizo la ulemavu wa mgongo wazi na kichwa kikubwa.

Shirikisho la Kimataifa la Kichwa kikubwa na Mgongo wazi Duniani (International Federation for Spina bifida and Hydrocephalus) lilizindua kampeni hizo kuhamasisha dunia kutambua umuhimu wa vitamini hiyo.

Kwa hapa nchini, asasi isiyo ya kiserikali ya Child Help Tanzania iliunga mkono jitihada za IF katika kampeni hizo kwa kutoa elimu kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali, hasa vyombo vya habari.

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi hiyo, Janet Manoni, katika taarifa yake, alisema ulemavu wa mgongo wazi unaweza kuzuilika iwapo jamii itazingatia ulaji bora wa mlo kamili hasa vyakula vyenye wingi wa vitamini ya foliki asidi. Imethibitishwa na wataalamu wa afya kuwa, kuna uwezekano wa kuzuia kwa takribani asilimia 72, matatizo yahusianayo na mishipa ya fahamu kutokana na jamii kuzingatia matumizi sahihi.

Njia hiyo inaelezwa kuwa inaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa uzazi wa watoto wenye ulemavu wa mgongo wazi, na hivyo kusaidia pia kupunguza idadi ya watu wenye ulemavu wa aina hiyo nchini.

Kampeni hizo zilishamalizika, lakini vyema wale ambao wamebahatika kufikiwa wakaona umuhimu wa kuzingatia kile walichopata ili kuwapo na matokeo chanya yatakayosaidia jamii kuwa salama.

Wataalamu wa afya wamekuwa wakihimiza wajawazito kuzingatia ulaji wa vyakula vyenye madini chuma, vitamini ya foliki na vitamini B12, vikiwamo vyakula vya asili ya wanyama kama nyama, maini, samaki, dagaa. Mbali na hivyo, vyakula vingine ni vile vinavyoboresha ufyonzwaji wa madini ya chuma mwilini vikiwamo vyenye vitamini C kwa wingi ambavyo ni matunda yenye uchachu kama vile machungwa, limau, ndimu na ukwaju.

Hata hivyo, imekuwa ikielezwa kuwa kwenye jamii, wapo baadhi ya watu ambao hawazingatii ushauri huo, hali ambayo inachangia kuendelea kuwapo wazazi wanaojifungua watoto wenye ulemavu huo.

Lakini kwa sababu kampeni zimefanyika za kuhamasisha umuhimu wa lishe bora, wiki moja maeneo mbalimbali nchini kupitia vyombo vya habari, mabango na vipeperushi, ni wazi elimu hiyo imesambaa.

Jambo la muhimu ni jamii yenyewe kubadilika na kuchukua hatua, kutokana na kwamba. wataalamu wa afya wanasema ulemavu huo unaweza kuzuilika iwapo jamii itazingatia na kula lishe bora.

Kampeni zimefanyika ambazo kimsingi zitakuwa zimekuza uelewa wa watu wakiwamo akina mama kama watakuwa wamezifuatilia, kwani watakuwa na uhakika wa uzazi wa watoto wenye afya bora.

Hatua hiyo pia inaweza kusaidia kuimarisha ustawi wa familia na kuipunguzia serikali mzigo mkubwa wa kuwekeza katika tiba kwa matatizo ambayo wakati mwingine yanaweza kuepukika, kwa kuzingatia lishe bora. Kwa kuwa baadhi ya Watanzania si wepesi wa kufuatilia taarifa katika vyombo vya habari au kusoma vipeperushi, magazeti na vitabu, basi ni vyema kuwakumbusha kuwa wazingatie elimu iliyotolewa katika kampeni hizo.

Kampeni hiyo, wajawazito wamekumbushwa kumeza vidonge vya madini chuma na vitamini ya foliki asidi kila siku wakati wa kipindi chote cha ujauzito ili kuepuka athari zitokanazo na upungufu wa virutubishi.

Siyo hapo tu, bali pia msisitizo mwingine ni wazazi na jamii kuongeza ulaji wa vyakula mchanganyiko na kiasi cha kutosha wakati wa ujauzito na kunyonyesha ili kusaidia kiumbe kilichopo tumboni kuwa salama zaidi.

Inaelezwa kuwa Tanzania, ni miongoni mwa nchi zenye vyakula vingi vyenye wingi wa vitamini ya foliki asidi, ila tatizo ni uelewa duni wa masuala ya lishe bora ambayo inasababisha kuendelea kuwapo ulemavu wa aina hiyo.

Lakini kwa vile asasi ya Child Help Tanzania imejitosa kuelimisha umma kuhusu umuhimu ya vitamini ya foliki asidi na ulaji bora ili kujenga jamii yenye afya na ustawi, hivyo ni vyema kuzingatia kilichoelezwa na wataalamu wa afya.

Pamoja na hayo, ninadhani kuna haja wadau wote wa mambo ya lishe bora kuendelea kuwekeza kwenye elimu ili kuiokoa jamii na uzazi wa watoto wenye ulemavu huo wa mgongo wazi na kichwa kikubwa.

Elimu inaweza kusaidia kukuza uelewa hasa kwa akinamama na wasichana wa umri wa kuzaa ili kuinua afya zao na pia kuwa na uhakika.

## SAFU/MAKALA

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tanzania tunahitaji ‘Spika Bora’ badala ‘Bora Spika’



Na Pascal Mayalla

**Wenzetu wazungu wanaita, ‘endorsement’, hivyo leo nafanya ‘endorsement’ yangu kumpata Spika Bora kwa kutumia udhaifu wa Spika aliyepita na makosa ya msaidizi wake huku nikipendekeza spika bora.**

SPIKA aliyepita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyejiuzulu hivi karibuni, hakuwa ‘Spika Bora’ bali ‘Bora Spika’, hivyo kujiuzulu kwake hakuna anayekusikitikia, kwa sababu ni neema.

Badala ya watu kusikitika tumempoteza spika bora, watu wanaolitakia mema taifa hili, wamefurahia kujiuzulu huko kwa sababu kunaleta fursa ya taifa kupata tena “Spika Bora” kama enzi za Mzee wa ‘Viwango na Kasi’, Samuel Sitta (SS - Standards and Speed). Lakini swali ni je, CCM, itatupatia “Spika Bora” au “Bora Spika?

Kwanza niombe radhi, wiki iliyopita nilisema tutazungumzia kitu kinachoitwa “karma” lakini kutokana na taifa letu kupitia katika changamoto ya kumtafuta mkuu wa mhimili wa Bunge, sisi watu wa habari tuna wajibu wa kulisaidia taifa letu kupata viongozi bora. Kwa kuonyesha udhaifu wa baadhi ya viongozi waliopita, udhaifu wa baadhi ya wanaotarajiwa sana na uimara wa baadhi ya waliojitokeza, ili katika uchaguzi wa Spika, tusirudie makosa yaliyopita na kwenye fursa ya kupata ‘Spika Bora’, tusifanye kosa tukachagua ‘Bora Spika’.

Nimesema Spika aliyepita hakuwa Spika Bora kutokana na utamaduni wa upatikanaji wa Spika kwa CCM. Pius Mswekwa alikuwa Naibu Spika wa Chief Adam Sapi Mkwawa, Spika Sitta alimshinda Msekwa kwa sifa, Anna Makinda alikuwa Naibu Spika wa Samuel Sitta, Spika Job Ndugai alikuwa Naibu Spika wa Makinda, hivyo utamaduni huu ukiendelea, baada ya Spika Ndugai kujiuzulu, anayetarajiwa sana ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson.

Kwa vile Spika Job Ndugai hakuwa Spika Bora, vivyo hivyo CCM wakiendeleza utamaduni wa kumteua Naibu Spika kuwa Spika, huko kutatupatia ‘Bora Spika’, mwingine. Kwa nini tupate tena ‘Bora Spika’ wakati tuna fursa ya kupata ‘Spika Bora’?.

Wenzetu wazungu wanaita, ‘endorsement’, hivyo leo nafanya ‘endorsement’ yangu kumpata Spika Bora kwa kutumia udhaifu wa Spika aliyepita na makosa ya msaidizi wake huku nikipendekeza spika bora.

Hata hivyo nitoe angalizo kwamba hii si kampeni kumpigia debe mtu yoyote bali ni uzalendo kwa taifa langu. Baada ya kuongozwa na ‘bora spika’, inapotokea fursa ya kumpata spika bora, sisi wenye jicho tunduizi la kuona matundu kwenye bora spika, tuyaonyeshe hayo matundu ili tuepuke kupata tena bora spika na kuangazia fursa za kupata spika bora kuuongoza mhimili wetu wa kutunga sheria.

Kuelekea uchaguzi mkuu wa 1995, Mwalimu Julius Nyerere, mwasisi wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, aliwahi kusema mtu yeyote mwenye sifa na vigezo, anaweza kuwa Rais wa Tanzania, lakini Rais Bora atatoka CCM. Baada ya nafasi ya Spika kuwa wazi, wamejitokeza watu wengi kuonyesha nia kupitia CCM na wote wanakidhi sifa na vigezo, hivyo kama tunataka kupata bora spika, mtu yoyote kati ya hao anaweza kuwa Spika. Lakini kama tunataka Spika Bora ni baadhi tu ya hao ndio wanaweza kutupatia Spika Bora.

Vikao vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) vitakutana wiki inayoanza kesho kufanya uteuzi wa majina matatu, kisha kikao cha wabunge wa CCM kitapiga kura kuchagua jina. Tunaiomba CCM kututeulia Spika Bora na kuwaomba wabunge wa CCM, kutuchagulia mgombea bora.

Uchaguzi wa Spika mpya, utafanyika kwenye mkutano ujao wa Bunge unaotarajiwa kuanza Februari Mosi, mwaka huu. Vyama mbalimbali vya siasa, vitateua majina ya wagombea wao, kila chama mgombea mmoja. Hivyo Mtanzania yoyote, kutoka chama chochote cha siasa, aliyekidhi sifa na vigezo, anaweza kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini kwa siasa za Tanzania, tukubali, tukatae, ile kauli ya Mwalimu Nyerere kuhusu urais wa Tanzania kuwa “Rais bora lazima atatoka CCM” ingali inaishi hata kwenye Uspika kuwa Spika bora wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima atatoka CCM.

Kama nilivyouanza mwaka huu, katika salamu zangu za mwaka mpya, kwa kusema huu ni mwaka wa mabadiliko na kuwaomba Watanzania tubadilike, kujiuzulu kwa Spika ni mpango wa Mungu kuleta mabadiliko katika mhimili huu pia baada ya Mungu kuleta mabadiliko kwenye mhimili wa utawala (executive). Sasa ni zamu ya mabadiliko katika mhimili wa Bunge. Dini zote zinatusisitiza tushukuru kwa yote, hivyo tushukuru hata kwa mabadiliko haya ya mkuu wa mhimili wa Bunge. Baada ya kutokea fursa hii, ni jukumu la Bunge letu kutupatia Spika Bora.

Kwa vile vyombo vya habari vina ushawishi mkubwa wa kuhamasisha jamii, wenzetu mfano Marekani, wao wana vyama vikuu viwili, The Democrats na The Republican. Kwenye uchaguzi mkuu wao, walifanya kitu kinachoitwa ‘endorsement’ kwa baadhi ya vyombo hivyo na watu mashuhuri na maarufu kumuunga mkono mgombea wa chama fulani. Mfano kuna watu, TV na magazeti, yalimuunga mkono Barack Obama na chama cha The Democrats.

Sisi Tanzania, ingawa nchi yetu ni vyama vingi vya siasa, kwa mujibu wa katiba, ukweli halisi Bunge la JMT, japo ni vyama vingi, kiuhalisia ni la chama kimoja CCM. Na nchi yetu kwa huku Tanzania Bara ni nchi ya vyama vingi lakini ukweli ni nchi ya chama kimoja CCM, kikizungukwa na vyama utitiri. Kwa mantiki hiyo, kama ni kufanya ‘endorsement’ ni ya mgombea wa CCM.

Nafasi ya kila chama kutoa mgombea ni nafasi moja tuu na kati ya wagombea wote waliojitokeza CCM, atakayechaguliwa kuiwakilisha CCM ni mtu mmoja na kati ya hao waliojitokeza CCM, ni mtu mmoja tu wa kutupatia Spika bora.

Kutokana na ukweli huo, swali ni je, CCM safari hii watatupatia Spika Bora au wataendelea kutupatia Bora Spika?

**Wasalaam.**

**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ni mpasuko dhahiri ajali ya Busega



Na Joseph Kulangwa

**Tukajiuliza wengine wale wa Timu Hiace walikuwa wakiagiwa wapi na nani? Kama Timu Cruiser ilipewa mpaka majeneza na kuratibiwa safari, je timu Hiace ilizikwa vipi na nani?**

WATANZANIA wameuanza mwaka huu kwa janga kubwa la ajali ya magari barabarani maeneo ya Busega mkoani Simiyu. Wakashuhudia wenzao 14 wakipoteza maisha.

Ajali hiyo mbaya ilikutanisha uso kwa uso, magari Toyota Land Cruiser STK 8140 mali ya serikali na Toyota Hiace T281DER mali ya watu binafsi, yani daladala kwa mkonga.

Inaonekana yote mawili yalikuwa mwendo kasi ndiyo sababu ajali yenyewe ikawa kubwa. Ajali ikazaa makundi mawili, kundi la Cruiser likaua sita na kundi la Hiace likaua wanane.

Kundi la Cruiser ndilo lilikuwa na kina Abel Ngapemba, Husna Milanzi, Anthony Chuwa, Steven Msengi na Johari Shani. Kundi la Hiace waliokufa ni Mnyonga Kaswalala, Lukanya Maduka, Agness Nyerere, Dotto Dossa, Anastasia William, Emmanuel Pastory na Samwel Ibrahim.

Wote hawa wametangulia mbele za haki, wote Watanzania wenzetu. Baada ya msiba huu tukasikia salamu mbalimbali kutoka kwa watu mbalimbali huku kundi la Cruiser likionekana kulemewa na salamu hizo.

Tukasikia salamu kutoka kwa viongozi wa kitaifa, mpaka akaenda Waziri mmoja kuhudhuria mazishi ya kimkoa yaliyofanyika viwanja vya Nyamagana, Mwanza, tukishuhudia majeneza sita tu uwanjani.

Tukajiuliza wengine wale wa Timu Hiace walikuwa wakiagiwa wapi na nani? Kama Timu Cruiser ilipewa mpaka majeneza na kuratibiwa safari, je timu Hiace ilizikwa vipi na nani?

Wakati habari za timu Cruiser zilianza kuhanikiza punde tu baada ya tukio la ajali kwa kuchukuliwa haraka haraka na kupelekwa hospitalini, kwa upande wa timu Hiace hatukusikia lolote.

Ikawa kana kwamba baada ya ajali wale wa timu Hiace walitoweka au kufukiwa na si kuzikwa kwa sababu hakukuwa na hafla yoyote ya kuagwa wala kusikia tu kuagwa seuze kuzikwa!

Hakika hata vyombo vya habari vikajitenga vikilalia upande mmoja wa wanahabari kuliko masikini wale waliojazana kwenye Hiace kwenda kujitafutia mkate wa kila siku lakini wakakutana na kadhia hiyo. Tunajiuliza nini kilijiri?

Kwa nini kuonekane ufa mkubwa vile kati ya timu Cruiser na timu Hiace? Je, kuna waliokuwa na thamani kuliko wenzao au nini mpaka taswira ijionyeshe kuwapo upendeleo na unyanyapaa? Tuache hili naamini siku zijazo tutakuwa makini na kujali utu wa kila mmoja.

Alipofika Waziri mwenye dhamana ya habari Mwanza kuaga, akapata fursa ya kuzungumza, akiwataka waajiri wa marehemu waliopewa heshima ya kuagwa, vivyo hivyo wapewe heshima ya kulipwa fedha zao ndani ya siku saba. Kongole kwake.

Lakini hatukusikia wale wengine timu Hiace wakisemewa na yeyote, kwamba pengine nao kama wana stahiki zao, wafanyeje au wafanyweje! Halikuwapo hilo, lakini yawezekana walisemewa na ndugu, jamaa na marafiki zao vijijini walikozikwa.

Tunaamini Waziri hataishia kufuatilia tu fedha za marehemu, lakini ataangalia mpaka kwa walio hai kama nao wanadai haki na maslahi yao, basi na ahakikishe nao wanalipwa, si mwenye nacho tu aongezwe, lakini asiye nacho naye apewe.

Mara tukamsikia mwenye dhamana ya usalama barabarani naye akihanikiza dhidi ya madereva wa serikali, akisema hawako juu ya sheria, hivyo watakapokiuka sheria ya usalama barabarani, basi mkono mrefu wa dola utawafuata na kuwaminya.

Tumwamini au tuache kwa kuwa ndiyo maneno ya kila siku. Tumeshuhudia madereva wa serikali wakikaidi sheria hizo na kukimbia barabarani wanavyotaka bila hata kusoma vibao barabarani.

Hufanya hivyo hata wakiwa na mabosi wao ambao ndio watunzi wa sheria hizo ambazo hawataki katu kuzifuata. Hiyo ndiyo sababu ajali nyingi zinahusisha magari ya serikali kwa kuwa kila wapitako hupigiwa saluti.

Msishangae kuwa kama madereva wa Hiace na Cruiser wasingepoteza maisha kwenye ajali ya Busega, pengine tungesikia kuwa mwenye makosa ni dereva wa Hiace kwa kuwa ni mnyonge, ndiyo sababu hatumsikii kazikwa wapi masikini huyo.

Hii ni ajali kubwa ya kwanza mwaka huu, iliyotuonyesha mpasuko mkubwa wa kinyanyapaa. Haitakuwa vyema hili kujirudia huko twendako kwamba wanahabari ni viumbe bora kuliko wakulima na wafanyakazi wanaopanda daladala! Hapana tuliangalie hili kwani sote ni sawa mbele za Muumba.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Ushiriki wanahabari ziara za viongozi utazamwe upya



Na Thobias Mwanakatwe

JANUARI 11, mwaka huu, tasnia ya habari ilipata pigo kubwa baada ya wanahabari wake sita mkoani Mwanza kupoteza maisha kutokana na ajali ya gari iliyosababisha vifo vya jumla ya watu 14.

Wanahabari hao ambao walikuwa wakienda katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, gari walilokuwamo aina ya Toyota Landcruiser liligongana na gari la abiria aina ya Toyota Hiace lililokuwa likitokea wilayani Busega mkoani Simiyu kwenda Mwanza mjini.

Baada ya ajali hiyo kutokea, Mkuu wa Wilaya ya Busega, Gabriel Zakaria, akiwa eneo la tukio, alisema gari la waandishi wa habari lilikuwa na waandishi saba waliokuwa kwenye msafara huo, watano kati yao walipoteza maisha papo hapo sambamba na abiria waliokuwa katika Hiace.

Aidha, DC Gabriel aliongeza kuwa watu wengine watatu katika majeruhi waliokuwa katika Kituo cha Afya cha Nasa, Busega wamepoteza maisha na kufanya idadi ya waliopoteza maisha kwenye ajali hiyo kuwa 14.

Kwanza, nianze kwa kutoa pole kwa wafiwa wote na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu majeruhi wote wanaoendelea na matibabu wapone haraka na kurejea kuendelea na majukumu yao. Kilichonisukuma kuandika hoja hii ni kutokana na kuzuka kwa mijadala mingi kwenye mitandao ya kijamii baada ya ajali hii kutokea.

Katika mijadala niliyofuatilia, nimebaini kuwa asilimia kubwa wamehoji ni kwa nini waandishi mara kwa mara ndio wamekuwa wakipoteza maisha kwenye misafara ya viongozi? Swali hili hata mimi siwezi kuwa na majibu nalo labda wahusika wanaweza kuwa na majibu sahihi. Katika tukio la Januari 11, ninachoweza kusema kijumla, nimesikitishwa sana na madhila yaliyowakuta waandishi wenzetu. Si mara ya kwanza kwa wanahabari kupoteza maisha kwenye misafara ya viongozi.

Mfano Julai 2018, mwandishi wa habari mwandamizi, Shadrack Sagati, alifariki dunia akiwa kweye msafara katika ajali iliyotokea eneo la Minkoto, Kijiji cha Kalembela, Chato mkoani Geita. Pia mwandishi wa habari na aliyekuwa Ofisa Habari katika Wiara ya Maliasili na Utalii, Hamza Temba, alifariki dunia katika ajali ya gari mkoani Manyara akiwa na aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Hamis Kigwangallah. Hiyo ni mifano michache lakini iko mingi ya waandishi waliopoteza maisha au kujeruhiwa wakiwa kwenye misafara ya viongozi.

Nafahamu si wakati sahihi wa kuzungumza chochote zaidi ya kuwaombea ndugu zetu Mwenyezi Mungu awapokee katika kuhitimisha safari yao ya maisha hapa duniani.

Wakati tukitafari na kuendelea kugugumia kwa majonzi, nashauri viongozi wa klabu za wanahabari kote nchini, wajaribu kukaa na viongozi wa mikoa kwa maana wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikao (RAS) kutazama namna bora ya waandishi wanavyotakiwa kushirikishwa kwenye mambo ya mkoa, hususan misafara au ziara za viongozi.

Nasema hivyo kwa sababu siku hizi iko tabia katika baadhi ya mikoa, utakuta ziara ya kiongozi fulani wa mkoa au wizara inafanyika na ratiba imetolewa siku mbili au tatu kabla huku Mkuu wa Mkoa akihakikishiwa maandalizi yote yamefanyika. Lakini si ajabu ukakuta 'logistics' za wanahabari likiwamo gari wanalotakiwa kupanda halijaandaliwa au kukaguliwa kabla ya safari.

Hali hii inasababisha hata madereva wanaotakiwa kusafiri na waandishi wa habari kutoandaliwa mapema. Si ajabu akaambiwa dakika chache kabla ya gari kuondoka. Naomba ieleweke kwamba sijamaanisha mkoa wa Mwanza ambako tukio lilitokea hawakuwa na maandalizi lakini natoa picha halisi na uzoefu juu ya hili. Hii inatokana na ukweli kwamba waandishi wanachukuliwa kama watu wa daraja la chini katika ziara hizi. Kimsingi, kitendo cha dereva kuambiwa muda mfupi kabla ya safari, kinafanya aanze kuhangaika kwa haraka kukagua gari lake lakini pia hata kwenda kujaza mafuta na wakati huo unakuta pengine msafara wa bwana mkubwa umeshaondoka. Matokeo yake dereva analazimika kukimbia ili akute msafara na hii ni hatari kwake na abiria aliowabeba.

Kitendo cha kutenga gari lenye uhakika, kuwaarifu waandishi siku tatu au muda mrefu kabla ya ziara ni masuala ya kitaaluma. Kwanza inasaidia mwandishi kujipanga kwa ajili ya safari na hata kutengeneza sura ya awali ya kazi anayokwenda kuifanya kichwani kwake na mwisho anakuja na habari bora kuliko zile za hapa alisema hivi na hapa akawataka.

Pia dereva anakuwa katika wakati mzuri kuendesha gari kwa sababu hakukurupushwa. Hata kwenye itifaki gari la wanahabari katika msafara linatakiwa kuwa katikati na si kama ilivyo sehemu nyingi hivi sasa gari kuwekwa mwisho. Sasa watapataje matukio muhimu katika msafara?

Hili jambo ni gumu kulizungumza hivi sasa lakini niwaombe viongozi wa klabu za wanahabari katika mikoa wajue kuwa dhamana ya maisha yetu inaanza kwa utetezi wa nafsi zetu na umuhimu wa kazi zetu. Tuache kufurahia kazi ya mwandishi iliyotoka kwenye gazeti, redio, TV na Online TV. Kwanza tutazame mazingira aliyopata hiyo habari na usalama wake.

Nimefarijika na kauli ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ambaye ameliagiza Jeshi la Polisi nchini kuchambua matukio yote ya ajali za barabarani kwenye misafara ya viongozi nchini ambayo yanachukua maisha ya wanahabari. Nape alitoa agizo hilo Januari 12, 2022 wakati akitoa pole kwenye hafla ya kuaga miili ya wanahabari watano mkoani Mwanza. Waziri Nape alisema baada ya kukabidhiwa taarifa ya uchunguzi mambo mengine yatafuata ikiwemo kubadilisha utaratibu mzima.

Pia alisema utaandaliwa utaratibu maalumu au itifaki rasmi ya namna bora ya ushiriki wa wanahabari kwenye ziara hizo. Kimsingi, kauli hii ya Waziri Nape imejibu kilio cha wanahabari wengi nchini kuwa mara nyingi hawapewi kipaumbele kwenye ziara hizo. Mara nyingi wanapewa magari yasiyo na viwango ambayo hayawezi kuendana na mwendo wa misafara yenyewe na kujikuta yakiachwa nyuma na pale wanapojitahidi kukimbia ili kuwahi matukio, wanaishia kupata ajali na baadhi kupoteza maisha.

Namwomba Mheshimiwa Waziri aisimamie vizuri kauli yake hii ili malalamiko haya ya wanahabari yapatiwe ufumbuzi kwani kimekuwa kilio cha muda mrefu. Kilio cha wanahabari kimsingi kilikuwa hakisikilizwi kilibaki kuwa kama kilio cha samaki ambacho machozi yake yanachukuliwa na maji. Haiwezekani wanahabari waitwe mhimili wa nne usiokuwa rasmi kutokana na jukumu lao muhimu kwa maendeleo ya taifa lakini hawathaminiwi kwenye misafara ya viongozi. Nimalizie kwa kuendelea kutoa pole kwa wanahabari wote nchini kwa kuondokewa na wenzetu, Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema. Ameni.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU WABARIKI WANAHABARI**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# NAMNA YA KUISHI NA WATUMISHI WA NDANI KATIKA FAMILIA -1



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

FAMILIA nyingi hukutana na changamoto nyingi za namna ya kuishi na watumishi wa ndani. Bila shaka kila mmoja wetu amewahi kuishi, kuhudumiwa au kumwona mtumishi wa ndani wa kike au kiume akifanya kazi kwenye familia fulani, kazi ambazo ni jukumu la wanafamilia husika. Hali kadhalika, watu wengi wanajua na kuguswa na madhila wanayopata watumishi wa ndani katika familia nyingi.

Katika makala hii, jaribu kujitathmini na kuona ni jinsi gani unaishi na mtumishi wako wa ndani. Swali la msingi la kujiuliza ni hili: Je, ninatenda haki na utu kwa mtumishi wangu wa ndani?

Wako baadhi ya watumishi wa ndani ambao hujisikia ni watumwa badala ya kuwa sehemu ya familia wanazofanyia kazi. Wengi wao hujisikia kutumikishwa na kunyanyaswa kwa kufanyakazi zisizo zao na zilizo nje ya uwezo wao. Kipato wanachopata hakiendani na majukumu mengi ya kikazi waliyo nayo katika familia husika.

Familia nyingi huamini kuwa mtumishi wa ndani anapaswa kufanya kazi yoyote na wakati wowote kwa sababu ni wajibu wake. Wengi wao hufanya kazi muda mwingi na hawapewi muda wa kupumzika. Ni watu wa kwanza kuamka alfajiri mapema na watu wa mwisho kulala.

Kama nilivyoeleza awali, watumishi wengi wa ndani hawapewi stahiki zinazolingana na majukumu yao katika familia nyingi wanazotumikia, tena baadhi yao hawalipwi kwa wakati. Halikadhalika, wengine hawalipwi chochote kwa kisingizio cha mwajiri kuwa anamtunzia fedha zake.

Baadhi ya waajiri wamejipa kazi isiyo yao ya kutunza fedha za watumishi wao wa ndani bila ridhaa na utashi wa mhusika. Hali hii husababisha watumishi wengi kuwa na mtazamo hasi na waajiri wao, hivyo, kutokupenda kuendelea kufanya kazi katika familia husika au kama ataendelea kuwapo, atafanya matendo maovu kama vile ukatili kwa watoto waliopo katika familia, udokozi, kujeruhi au kumuangamiza mwajiri mwenyewe.

Hata hivyo, kwa upande mwingine, baadhi ya watumishi wa ndani hawajitambui. Wengine ni wajeuri, wavivu, si waaminifu, watovu wa nidhamu, watu wa manung'uniko, hawana shukrani kwa waajiri wao kutokana na makuzi katika familia walizotoka. Ukweli huu uwasaidie wanafamilia kuchukua tahadhari na kuwa makini wanapoishi na watumishi hawa. Ifahamike kuwa watumishi wa ndani ni watu ambao malengo yao yanatofautiana na sababu zilizowasukuma kuwa watumishi wa ndani hutofautiana vile vile.

Pamoja na upungufu huo, bado umuhimu wa kuwapo kwa watumishi wa ndani upo pale pale, hasa kwa waajiriwa, waliojiajiri na wastaafu. Ni ukweli usiopingika kuwa, hali hizi zimewasukuma watu wengi kuajiri watumishi wa ndani ili wawasaidie majukumu mbalimbali katika nyumba na familia zao.

Hali kadhalika, wapo baadhi ya wanandoa ambao majukumu yao ya kikazi huwafanya kutopatikana nyumbani mara nyingi. Safari nyingi za kikazi na kibiashara nje na ndani ya nchi zimewafanya kutokuwa na muda na nyumba zao, hivyo, kulazimika kuajiri watumishi wa ndani.

Kwa upande mwingine, uvivu na uzembe wa baadhi ya watu vimewasukuma kuajiri watumishi wa ndani. Baadhi ya watu ni wavivu na wazembe wa asili na kimakuzi. Wengi wao wameshindwa kuwajibika katika nyumba zao kutokana na uvivu na uzembe.

Majukumu yao yote wamewaachia watumishi wao wa ndani ikiwa ni pamoja na jukumu la malezi ya watoto na kutunza nyumba. Hii imesababisha watoto wengi kuwa na malezi ya watumishi wa ndani zaidi kuliko wazazi wao hali inayopunguza thamani ya wazazi kwa watoto wao.

Wazazi wanapokuwa wavivu na wazembe huwabomoa watoto wao kimakuzi. Uvivu na uzembe wao hutengeneza kizazi cha watu wavivu na wazembe katika familia na jamii. Watumishi wanapoachiwa majukumu yote ya ndani, wengine hujisahau na kujiona wanayo haki ya kuwa warithi wa mali na mabosi wao.

Kuanza kwa uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanandoa na mtumishi wake wa ndani kunaweza kusababishwa na mazingira kama haya. Mtumishi wa ndani anakuwa anatekeleza majukumu ya kifamilia kiasi cha kupitiliza. Hali hii huzaa migogoro ya ndoa isiyoisha na kutokuaminiana kwa wanandoa. Chanzo kikuu cha tatizo kinakuwa ni kutokuwajibika katika ndoa.

Nini kifanyike kukabiliana na changamoto za watumishi wa ndani? Fuatilia Jumapili ijayo

**■Mch.Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

MAISHA
JANUARI 16, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14

**'BUTTER CHICKEN'**


**Furahia kuku wa minofu**



Ukurasa 15

## NYUMBA:

Dondoo za kusafisha bafu na choo katika nyumba yako




## KATUNI

Ukurasa 16





MIKONO LAINI

# Namna ya kulainisha viganja vyako

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | L | A | A | N | A |
| ■ | A | ■ | ■ | Y | ■ |
| M | W | A | ■ | U | ■ |
| ■ | A | ■ | I | N | A |
| ■ | M | ■ | ■ | G | ■ |
| S | A | U | M | U | ■ |


## AMSHA AKILI



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
AKA, PEA, KINGA, DENGE, GEREZA, DUKANI

## WATOTO

# PAKA RANGI




CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Ibrahim alikuwa na mama yake sebuleni akisaidiwa kusoma kitabu cha wanyama. Alikuwa akisoma hadhithi ya mama Simba na mtoto wake, Ibrahim alipenda sana hadithi ile na alianza kumuuliza mama yake maswali.

Ibrahim: mama hivi huyu mtoto wa simba atakuwa mkubwa kama akiwa na mama yake?

Mama: Ndio mwanangu, mama yake atampa ulinzi na kumfundisha uwindaji wanyama.

Ibrahim: Kwa nini, wakati mwalimu alitufundisha kwamba mtoto kwa mama huwa hakui?

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu, unamaanisha kwamba hataka iweje mtoto akiwa kwa mama yake ni lazima atapewa maelekezo mema, hivyo hana budi kuyasikiliza na kuyafuata.

SWALI
Afrika Mashariki inapakana na bahari gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Usione kwa kutumia macho ya mtu mwingine

KARIBU msomaji wangu katika sehemu ya pili ya mada yetu, mwaka huu 2022 unaona nini mbele yako? Huu ni mwaka wa kutumia macho yako mwenyewe uweze kufanikiwa.

Mambo ya Mungu yana kanuni. Nilisema mada iliyopita kwamba mwisho wa kuona kwako ndio mwisho wa utendaji wa Mungu katika maisha yako! Huwezi kuona kidogo utarajie kupata makubwa.

Mtu anaweza kusema, mimi naona nafungua kibanda cha mamalishe, lakini ndani yake anasema natamani kuwa na hoteli au ofisi kubwa. Tayari unaona kibanda kidogo halafu unawaza ningekuwa na hoteli kama ile ya fulani.

Yatupasa kutambua kwamba hakianzi kitu kwa macho ya mwili, kinaanzia ndani ya moyo wako. Chochote unachokiona ndani ya moyo ndicho kitakachokuwa. Ukiwaza unaweza, itakuwa hivyo. Ukiona ushindi, itakuwa na ukiona una kufa kufa iwe ni kimwili au kiuchumi, itakuwa hivyo.

Mtu mmoja atasema; unajua watu wanafunga biashara sana. Maana yake ni kwamba wewe unaona kwa jicho la mtu mwingine. Nabii Yeremia aliulizwa na Mungu, "Unaona nini?" Naye akajibu alichoona na Mungu akamwambia, umeona vema.

Uko uwezekano wa mtu kuona kitu kwa jicho la mtu mwingine si kwa macho yake. Mungu anataka uone kwa macho yako mwenyewe. Kuona kwa macho ya watu wengine maana yake mtu anaona uoga.

Jamaa atasema mimi nawaza, naona nikifanya biashara fulani nitapata fedha. Kisha anamuuliza rafiki yake, wewe unaonaje? Anamjibu, yuko fulani alifanya hiyo biashara akafilisika, hivyo hiyo biashara utapata hasara na utakuja kuniambia.

Na wewe kwa kusikia hivyo unaanza kurudi nyuma, unaogopa kuendeleza wazo lako. Hiyo maana yake ni kwamba umeona kwa kutumia macho ya mtu mwingine. Pengine kwa kujisimamia mwenyewe na kuchukua hatua kwa kile ulichokiona mbele yako ungetimiza ndoto yako.

Huu ni mwaka wa kutumia macho yako ndani ya moyo wako. Kwamba mwaka huu macho yangu hayatakuwa vile vile. Kataa mwaka hadi mwaka kubakia vile vile. Kataa roho ya kudumaa inayorudisha nyuma maendeleo.

Kudumaa maana yake ni nini? Ni ile hali ya kutokuongezeka kimafanikio, kihuduma, kiafya, kielimu na kadhalika. Hii ni roho inayomfanya mtu asiwe na mawazo mapya, na pale unapokosa wazo jipya ndipo maisha yako yanapoanza kuharibika. Kudumaa na umasikini ni watoto mapacha!

Kudumaa ni pale mtu alikuwa amepiga hatua mbili mbele, halafu anashangaa unarudi nyuma. Hata hivyo, upo uwezekana ukabakia pale pale huku mtu mwingine akipiga hatua kwenda mbele.

Sasa wewe unaona nini mwaka huu? Unaona ukipiga hatua za mbele au za kurudi nyuma, au unabakia hapo hapo? Unachokiona ndicho utakachokipata, ukiingiwa woga na kujaa hofu ndani yako ukasema haiwezekani, ni kweli haitakaa iwezekane!

Lazima uchukue maamuzi magumu mwaka huu. Huu siyo mwaka wa kawaida kwani tunahitaji miujiza kupita kawaida. Lazima uanze kuwaza mambo makubwa.

Unaingiza Sh.3,000 kwa siku halafu matumizi yako ni Sh. 10,000. Kwa nini usiwe na madeni? Ni kweli zipo roho za madeni zinaweza kukuandama. Unatoka kwa huyu umemkopa, kisha unakwenda kwingine unachukua mkopo unakwenda kulipia deni lingine.

Yupo baba mmoja ni mwalimu ambaye mshahara wake kwa mwezi ilikuwa ni sh.600,000/= lakini alijikuta anabakiwa na Sh. 23,000 tu kutokana na kulipa madeni ya mikopo.

Nini kilimtokea? Alikopa benki ya NMB, kisha akaenda kukopa benki ya CRDB. Baada ya pale mwalimu yule akaenda kwa watu binafsi kukopa ambako alikabidhi pia kadi yake ya benki. Akawaambia nikopesheni mwisho wa mwezi mtachukua deni lenu. Akawapa hadi namba ya siri ya akaunti yake.

Katika utaratibu huo, ndipo mwisho wa siku akawa anabakiwa na Sh .23,000 kwenye akaunti hadi madeni yote yalipoisha. Jamaa huyu ambaye pia alikuwa na roho ya ulevi, aliendekeza pia roho ya madeni ikamtawala.

***Mpenzi msomaji, tafakari maisha yako. Ona kitu cha manufaa siyo hasara mbele yako. Naamini umejifunza jambo hapo . Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Serikali ifuatilie usajili wa laini kiholela kuepusha hatari

KILA anayemiliki laini ya simu anatakiwa kusajili kwa alama za vidole kwa namba ya kitambulisho cha taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA. Pia kwa mujibu wa sheria, mtu haruhusiwi kusajili laini mbili za kampuni moja ya simu na kama anataka kufanya hivyo, anatakiwa kujaza fomu maalumu ya kueleza kwa nini anataka kumiliki zaidi ya laini moja.

Usajili wa laini ulianza wakati wa serikali ya awamu ya nne na tulielezwa kusajili kutasaidia kutambua wezi, matapeli, kuepusha matumizi mabaya ya simu kama kutukana na kudhalilisha watu na usalama wa nchi kwa ujumla.

Mwitikio ulikuwa mkubwa kwa kila mtu kuhakikisha anasajili laini ya simu huku serikali ikisisitiza bila kusajili, mtu hawezi kutumia na mfumo hautaruhusu kusajili zaidi ya laini moja kutoka kampuni moja.

Kwa ujumla, usajili ni jambo jema hasa katika kudhibiti matumizi mabaya ya laini za simu hasa kwenye matukio ya ujambazi, wizi, ukatili na mengine ambayo hayastahili kama matusi na udhalilishaji mwingine.

Hali ni tofauti kabisa kwa kuwa unaweza kupata laini pasipo kusajili kwa jina lako, kitambulisho wala alama za vidole vyako na ukaendelea kuitumia bila tatizo lolote.

Unapokwenda wanakosajilia laini, unawaambia nataka mnisajilie laini lakini sina kitambulisho na sitaki alama yangu ya vidole itumike. Unachotakiwa kufanya ni kutoa fedha kidogo halafu ndani ya muda mfupi unapewa laini yako ambayo unaweza kuitumia upendavyo.

Wako watu wengi wanatumia laini ambazo hawajasajili kwa alama wala vitambulisho vyao, kiasi cha wengine kutumia kutapeli watu kwa kuwa wanahakika hawawezi kukamatwa maana wamesajili kwa majina mengine.

Kwa sasa, wako wanaotoa tangazo la jambo fulani kama mikopo kwa kutumia kampuni yenye jina kubwa na wanaweka namba ya simu ambayo ukipiga inapatikana na mhusika bila wasiwasi anajieleza mambo ambayo lengo lake ni kutapeli watu.

Wengine wanatuma ujumbe mfupi wa "ile fedha tuma kwenye namba hii" na wengine kutishia kuwa mwanao amelazwa hospitalini au amepata matatizo. Wote hao wanatumia laini za simu kukamilisha mambo yao. Mwaka jana wakati wa bunge la bajeti, baadhi ya wabunge walilalamikia utapeli unaofanywa kwa sasa na wengine kueleza namna walivyotapeliwa fedha nyingi.

Mara nyingi matukio haya hutokea pale simu ya mtu inapokuwa na fedha nyingi, jambo linalozua maswali mengi kuwa wanajuaje huyu mtu kwa sasa ana fedha kwenye laini yake? Usalama wa laini za watu uko wapi kama taarifa zao zinavuja kirahisi?

Aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, (kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari), alisema serikali inaandaa utaratibu wa kuhakiki laini za simu nchini na zitakazobainika kutumika ndivyo sivyo, zitafutwa.

Alisema uamuzi huo una lengo la kupambana na uhalifu mtandaoni ambao kwa sasa umeshika kasi. Na katika mjadala wa bajeti, wabunge wanne walieleza walivyotapeliwa na kuitaka serikali kuchukua hatua.

> “ **Wako watu wengi wanatumia laini ambazo hawajasajili kwa alama wala vitambulisho vyao, kiasi cha wengine kutumia kutapeli watu kwa kuwa wanahakika hawawezi kukamatwa maana wamesajili kwa majina mengine.**

Hadi Mei, mwaka jana, laini za simu zinazotumika ziliongezeka kutoka 48,939,530 mwaka 2020 hadi 53,063,085 Aprili, mwaka jana, sawa na ongezeko la asilimia 10.8.

Pia laini za simu kwa njia ya kibiometriki hadi Aprili 2021 zilikuwa 51,108,886 ikiwa ni zilizosajiliwa kwa kitambulisho cha Mzanzibar Mkazi na kitambulisho cha mpiga kura ni 1,954,199.

Kwa ujumla, ni lazima hatua zichukuliwe ili maana ya usajili wa laini iwapo, tofauti na hali ilivyo sasa. Matukio ya utapeli yanaongezeka na watu wanatumia laini za simu bila woga wowote na kusajili laini kwa kitambulisho feki na ni jambo la kawaida kabisa au kupewa laini ya jina lingine.

Ni muhimu sana umuhimu wa vitambulisho wa taifa ukaonekana kuliko kuwa na vitambulisho vingi ambavyo bado havimsaidii mtu. Huu ni mjadala wa siku nyingine.

***Mungu ibariki Tanzania***















Sherehe ya kumbukumbu ya jubilei ya miaka 25 ya ndoa kati ya bwana William Wesiwasi na bibi Anne Wesiwasi, misa ya shukrani ilifanyika mwisho wa wiki katika kanisa Katoliki la Parokia ya Mt .Petro Mtume Swaswa Jimbo Kuu la Dodoma na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika ukumbi wa Vijana.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo




## TAI SHINGONI

# HIVI NDIVYO INAVYOFUNGWA

IDADI kubwa ya vijana wa kiume katika kizazi cha sasa hawajui kabisa namna ya kufunga tai na pindi inapotokea wanahitaji kuvaa wanatumia nguvu kubwa kutafuta msaada kwa watu wengine.

Baadhi hulazimika kuwaomba wazazi, walezi wao au baadhi ya watu wanaojihusisha na mavazi kuwasaidia.

Hata hivyo, kuna baadhi ya Wanaume wengi hawapendi kufunga tai kwa sababu wanahisi kama hawapati pumzi na hivyo huchukia kuvaa.

Ikiwa una tatizo hilo, hakikisha unavaa shati lenye kola pana ili inapokuwa ya ukubwa unaofaa huenda usitambue kwamba umefunga tai.

Naam, tai yaweza kumwongezea mwanamume adhama na kumfanya aheshimike.

**Jinsi ya kufunga tai kwa fundo la kitanzi**

1 Anza na ncha ya tai iliyo pana karibu sentimeta 30 chini ya ncha nyembamba, na kuizungusha kwenye upande mwembamba, ukiirudisha upande wa chini.

2 Izungushe tena ncha pana, na kuipitisha kwenye pindo.

3 Ukiwa umeshikilia sehemu ya mbele ya fundo bila kuikaza kwa kidole cha shahada, vuta upande mpana ndani ya pindo kuelekea mbele.

4 Kaza fundo polepole, ukishikilia upande mwembamba na kutelezesha fundo kwenye kola.

***Kwa msaada wa mtandao***

UREMBO

**Na Mary Geofrey**



MIKONO LAINI

# Namna ya kulainisha viganja vyako

MOJA ya athari zinazowapata wanawake walio hodari na kazi za nyumbani ni kuwa na viganja vya mikono vigumu au vikavu.

Tatizo hilo hutokana na ufanyaji wa kazi nyingi kama kufua kwa maji na sabuni, kuosha vyombo, kusafisha nyumba,kubadili watoto nepi na kupika.

Hata hivyo, ni wajibu wa kila mwanamke kuwajibika bila kuangalia mikono yake, kwani ukiwa mwangalifu mikono yako inakuwa salama na ulaini unabaki palepale.

Unatakiwa kuchukua hatua muhimu baada ya kazi zako na baadhi ya njia za kuchukua ni kama zifuatazo.

Chukua chombo weka chumvi kiasi na weka mafuta ya mzaituni.

Weka sabuni ya maji ya kuoshea mikono, tumia aina unayoipenda inaweza kuwa ya kukinga bakteria au yoyote ya maji.

Ni vizuri kutumia sabuni ya maji sababu hautaosheka vizuri mikono sababu maji na mafuta hayachanganyiki.

Kausha mikono yako vizuri, kisha weka mchanganyiko huo kwenye viganja vyako kisha sugua pole pole, kiasi cha kijiko cha chai. Sugua ndani na nje ya viganja na ndani ya vidole na kucha.

Osha kwa maji ya uvuguvugu, kausha mikono kwa kutumia taulo kavu, pakaa lotion ya mikono.

**Mambo ya kuzingatia**

Usifanye mara moja ukategemea utapata matokeo ya kudumu.

Tumia baby oil au lotion kabla ya kulala au tumia zile zinazotengenezewa na mimea zaidi.

Acha lotion kwa dakika kumi (10) kwenye viganja, ile leya ya juu ya ngozi itanyonya mafuta na itaweka unyevunyevu ndani ya ngozi.

Fanya hivi mara mbili kwa wiki na vaa gloves au plastiki wakati unafanya kazi kama kuosha vyombo.

Tumia Vaseline kwa mikono mikavu zaidi unaweza kulala na gloves ukiwa umepakaa lotion.

Usiache mikono kwenye maji baridi kwa muda mrefu, huondoa mafuta na unyevu wa asili mikononi.

Mwisho

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

‘BUTTER CHICKEN’

# Furahia kuku wa minofu

KUKU wa minofu anayeokwa kwa siagi maarufu kama ‘Butter Chicken’ ni chakula kitamu ambacho kinaliwa wakati wowote na mazingira tofauti.

Licha ya chakula hiki kuonekana kwa wingi katika hoteli za kifahari, lakini unaweza kupika mchuzi, kuchoma au kukaanga wewe mwenyewe na ukafurahia na familia yako.

**Mahitaji**

Kuku kilo moja, asiye na ngozi wala mifupa, limao moja, chumvi kijiko kimoja cha chai, pilipili manga ya kusaga vijiko vitatu vya chakula, tangawizi iliyosagwa kijiko cha chai na majani ya bay tatu.

Mdalasini uliosagwa kijiko kimoja cha chai, cardamon kijiko kimoja cha chai, butter vijiko vitatu vya chakula, vitunguu maji viwili, vitunguu saumu vijiko vitano vya kula, giligiliani vijiko viwili vya chai na cumin kijiko kimoja cha chai na garam masala kijiko kimoja cha chai

Mahitaji mengine ni cayenne pepper kijiko kimoja cha chai, corn starch kijiko kimoja cha chai, mafuta ya mzaituni kikombe kimoja cha kahawa na nyanya ya kopo vijiko viwili vya chakula na maziwa mgando vijiko viwili vya chakula.

Andaa nyama ya kuku, isafishe vizuri iweke pembeni, chukua pilipili manga, tangawizi, majani ya bay, mdalasini, cardamon, maziwa mgando, vitunguu maji, vitunguu saumu, giligilian, cumin, garam masala, cayenne pepper na nyanya ya kopo.



**Namna ya kuandaa**

Chukua blenda weka hivyo vitu vyote kisha saga, hakikisha vimelainika kabisa na viungo vimechanganyikana vizuri.

Weka pembeni, chukua kuku mkate vipande vyenye umbo la mche mraba na chukua bakuli kubwa, weka kuku chukua ndimu kamulia, weka na chumvi.

Mwagia mafuta ya mzaituni kwenye kuku, changanya vizuri mpaka uone mafuta yameenea vizuri na chukua ule mchanganyiko ulioublendi mwagia kwenye kuku, weka na cornstarch, kisha changanya kwa ufasaha mpaka uone kuku kaenea viungo.

Ukimaliza weka kwenye jokofu kwa saa moja, mtoe kuku mpake siagi changanya kisha rudisha tena kwenye jokofu.

Muache akae usiku mzima au masaa nane. Mtoe chukua siagi paka kwenye chombo utakacho okea kisha panga kuku wako vizuri, au unaweza choma, pia paka siagi kwenye wavu wa kuchomea.

Choma huku unamgeuza na unampaka butter mpaka aive, na kwenye oven fanya hivyo hivyo.

Dakika 45 zikifika mtoe atakua kaiva. Jirambe. Nina uhakika huyu kuku atafurahiwa na familia yako.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# DONDOO ZA KUSAFISHA BAFU NA CHOO KATIKA NYUMBA YAKO

USAFI wa nyumba mara kwa mara ni nguzo kubwa ya kuistawisha na kuipendezesha kwa kiwango kikubwa. Nyumba isipofanyiwa usafi wa mara kwa mara, huchakaa mapema na hata kuharibika kabisa.

Usafi wa nyumba ninaozungumzia ni wa sehemu zote za nyumba na si katika eneo la sebule, chumba cha kulala au cha kupikia tu.

Nafahamu kwamba huenda kila mtu ana mbinu yake ya kusafisha nyumba yake lakini leo nitapenda kukuongezea baadhi ya dondoo zingine za namna ya kusafisha nyumba yako, hususani katika sehemu ya bafu na choo.

Nataka tujifunze namna ya kusafisha kuta katika sehemu hiyo ya bafu, sinki, bomba, eneo la kuogea na bakuli la choo.

Kabla ya kuanza kusafisha bafuni, kwanza ondoa vitu vyote vya kuhamishika kama vile vizulia, tenga la nguo chafu, meza au kabati na ndoo ya taka wakati huo ukihakikisha dirisha linakuwa safi.

Baada ya hapo, unaweza kuondoa buibui kwenye kona za dari ikifuatiwa na kufuta vumbi mlangoni katika sehemu ya ndani na nje.

Wakati wa kusafisha, ni vyema kuanzia juu na kushuka chini ili kuruhusu taka za vumbi na buibui zimwagike sakafuni kwa ajili ya kusafisha mwishoni na unapaswa kutumia kitambaa kufutia au fagio.

Unaweza kumiminia sabuni za kusafishia kwenye bakuli la choo na kuiacha kwa dakika kadhaa ili uchafu ulainike.

Unaweza pia kuweka dawa ya unga wa kusafishia katika sehemu zenye uchafu ili iwe rahisi wakati unasugua.

Ni vyema ukazingatia maelezo ya dawa ya kusafishia ili kuwa na uhakika unatumia kiasi sahihi ambacho hakiwezi kuharibu.

Katika kuta za bafu pia unapaswa kupaka sabuni au dawa zingine za kusafishia endapo zitakuwa za marumaru na kwa kutumia sponji au brashi, unaweza kusugua sehemu uliyoweka sabuni hiyo huku ukihakikisha unaiisuuza kuondoa michirizi yote michafu. Kama ukuta ni wa karibia na sinki au bakuli la choo ukaushe kwa taulo.

Ni muhimu kuvaa glovu wakati wa kusugua kwani baadhi ya dawa na sabuni zinaweza kuchubua ngozi.

Pia mswaki wa zamani usiotumika unaweza kutumika kuondoa uchafu kutoka eneo la kati ya bomba na mishikio yake na unapaswa kuepuka kutumia brashi la kusugulia bakuli la choo, kusugulia sinki kwa sababu unaweza kusambaza maradhi.

Safisha kioo kwa kutumia ama maji na taulo au dawa ya kusafishia vioo na taulo.

Safisha nje ya choo ukianza na ile sehemu ya juu ya kuvuta maji. Kwa taratibu unaweza kuendelea kusafisha eneo lote la nje ya choo ambalo ni pamoja na mfuniko na eneo la chini ya sehemu ya kukalia na kupafuta na taulo.

Kwa upande wa sakafu, hakikisha usafi wako unaanzia sehemu zilizojificha hadi zile za wazi na ni vyema kusafisha vumbi na uchafu wote ulio chini eneo la choo lilipounganika na sakafu.

Subiri kidogo sakafu ikauke ndipo urudishe vile vitu ulivyoondoa awali.

Ili kuweka bafu lako katika hali ya usafi na kupunguza kutumia nguvu kubwa ya kusafisha, unatakiwa uwe unasafisha maeneo mbalimbali ya bafu mara baada ya kuyatumia.

Ni vyema kusafisha bakuli la choo kila baada kulitumia eneo la sinki pamoja na eneo la kuogea hata kama sehemu hizo hazionekani kuchafuka.



## Namna ya kupamba ngazi kwa vitu vya asili



WATU wengi wanapenda kuweka mapambo katika ngazi ya kuingilia ndani ya nyumba zao. Licha ya kuweka mandhari ya kupendeza, pia mapambo katika ngazi yanaonyesha umaridadi wa mtu husika.


Kutokana na umuhimu wake, tunakupa njia ya kupendezesha ngazi kwa kuweka mapambo asilia.

1: Vyungu ni baadhi ya mapambo asilia vinavyoweka mtazamo mzuri wa nyumba yako, weka vyungu vya rangi mbalimbali ili kumfanya mtu kuvutika na muonekano wake.

2: Kwa wenye uwezo, vyuma vilivyopambwa maua ni sehemu ya kupamba ngazi zao. Chagua urembo unaokuvutia na kama huwezi mshirikishe mtaalamu wa kupamba nyumba ili kupata matokeo mazuri.

3: Pamba ngazi kwa makopo ya maua ya asili. Hili ni mojawapo linalovutia zaidi hasa unapoweka maua na majani ya rangi tofauti.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
FANYAFANYA NIKISHINDA USPIKA NAKULETEA MZIGO
MLEVI ASIYEJULIKANA HAKOPESHWI 'POMBE'
NASKIA UMEACHA MAAGIZO UKIJA UKUTE KODI YAKO?
NAANZAJE KWA MFANO!
HIVYO VIKUMBO VYA KUGOMBEA KITI CHA 'MJENGONI' WALA HAUNISHITUI!
MH! USTAKE NSEME
'CHA MGEMA HULIWA NA MLEVI'
NIPE KWANZA UBUYU MPYA NIPATE 'STATA' YA KUKUSUKA VIZURI
UNA SHING' NGAP?
AGIZA LIPA TUNYWE TUSHEREHEKEE...YAANI WEWE NI SUPIKA MTARAJIWA HAWACHOMOKI
KUNYWA KWA BIDII
ILE HELA UNGENILIPA KWANZA NDIO UFANYE ULICHOKIFANYA!
NIKISHINDA USINIITE MHESHIMIWA UNANIELEWA?
MAKOSA MENGINE WANGEJENGA MAGEREZA SERIKALI ZA MITAA ILI MSITUMALIZIE HEWA
EBO! ACHA DHARAU WEWE! 'KUMKATA KIBAO MKEO UNAONA KAZ NDOGO?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MASIKINI HAISHIWI MISEMO

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaituhumu Urusi kujiandaa kuivamia Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imeituhumu Urusi kuwa inapanga kufanya vitendo vya uchochezi ili kutafuta kisingizio cha kuivamia Ukraine.

Msemaji wa wizara ya ulinzi wa nchi hiyo, John Kerby, alisema watendaji wa Urusi walikuwa wakipanga operesheni aliyoiita bendera ya uwongo, ili kuruhusu kuishutumu Ukraine kwa kuandaa shambulio.

Hata hivyo, Urusi imepuuza tuhuma hizo zilizotolewa juzi.

Majibizano hayo, yanakuja baada ya wiki moja ya mazungumzo kati ya nchi hizo mbili kwa lengo la kutuliza mvutano.

Hata hivyo, juzi Ukraine iliishutumu Urusi kwa kuhusika na udukuzi wa tovuti kadhaa rasmi.

Kabla ya udukuzi huo, ujumbe ulionekana katika kompyuta ukiwaonya Waukraine kujitayarisha kwa mabaya, hata hivyo hitilafu hizo zimerejeshwa ndani ya saa chache.

Marekani na Nato wamelaani shambulizi hilo na wametoa msaada kwa Ukraine.

Urusi haijatoa tamko lolote kuhusu udukuzi huo, lakini msemaji huyo, aliwaambia waandishi wa habari kuhusu kile alichosema ni mipango ya Urusi.

"Imeweka tayari kundi la watendaji kufanya kile tunachoita operesheni ya bendera ya uwongo, operesheni iliyopangwa kuonekana kama shambulio dhidi yao au watu wanaozungumza Kirusi nchini Ukraine kama kisingizio cha kuingia," alisema.

Ofisa huyo alisema wahudumu hao walipewa mafunzo ya vita vya majini na kutumia vilipuzi kutekeleza hujuma dhidi ya waasi wanaoiunga mkono Urusi.

Wizara ya Ulinzi ya Ukraine, ilisema vitendo hivyo vinapangwa dhidi ya vikosi vya Urusi vilivyopo kwenye eneo lililojitenga la Moldova.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov amejibu kwa kusema ripoti hizo hazina msingi wowote na hazijathibitishwa na chombo chochote.

**BBC**



Baadhi ya waandamanaji walionyesha uungaji wao mkono kwa serikali ya kijeshi ya Mali juzi. **PICHA: DW**

# Maelfu waandamana kuunga mkono serikali ya kijeshi

**BAMAKO,** MALI

MAELFU ya raia wa Mali wameandamana kuonyesha uungaji mkono wao kwa serikali katika kipindi cha mpito kilichotangazwa na wanajeshi, na kulaani vikwazo vya kimataifa.

Maandamano hayo yaliandaliwa na kuratibiwa na watawala wa kijeshi, kama mbinu ya Waziri Mkuu wa mpito Choguel Maiga kutuma ujumbe kwa mataifa yaliyoiwekea vikwazo serikali yake.

Wiki iliyopita, wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) waliiwekea vikwazo nchi hiyo, baada ya watawala wa kijeshi kuahirisha uchaguzi uliopangwa kufanyika Februari mwaka huu na kupeleka mbele hadi Desemba 2025.

Kulingana na mwandishi wa DW nchini Mali, ni mara chache sana kwa waandamanaji kukusanyika katika uwanja wa Uhuru mjini Bamako, ulikojumuika umati mkubwa wa waandamanaji.

Jukwaa kubwa lilijengwa katikati ya mnara wa ukumbusho wa Uhuru ili kukaribisha hotuba za Imam Oumarou Diarra, ambaye alifanya mahubiri ya Ijumaa kwa waumini wa Kiislamu.

Dalili za chuki dhidi ya Ufaransa na ECOWAS na kupendelea ushirikiano kati ya Mali na Urusi pia zilikuwepo, kama vile mabango yenye picha ya Kanali Assimi Goita na mamlaka ya mpito ya Mali.

Hata hivyo, wanawake waliungana katika uhamasishaji huo wa kukemea vikwazo. Wengi wao walishiriki maandamano wakivalia vitambaa vyeupe ambalo ni vazi la kitamaduni.

Maandamano hayo yaliishia hali ya sherehe iliyoshamiri sauti za vuvuzela ambazo zilihanikiza kila mahali mjini Bamako.

Ufaransa ambayo ni mkoloni wa zamani wa Mali pamoja na nchi nyingi katika jumuiya ya ECOWAS, imeunga mkono vikwazo dhidi ya Mali. Umoja wa Ulaya na Marekani pia zimekaribisha vikwazo hivyo na shinikizo dhidi ya wanajeshi walionyakua madaraka.

**DW**

# UN yaonya mauaji ya kiholela Tigray

**WASHINGTON,** MAREKANI

Umoja wa Mataifa umesema takriban raia 108 wameuwawa mwanzoni mwa mwaka huu, katika msururu wa mashambulizi ya anga katika eneo la Tigray Kaskazini mwa Ethiopia.

Katika ujumbe kupitia mtandao wa twitter, Katibu Mkuu wa Umoja huo Antonio Guterres , alisema kuwa wito wake kwa pande husika katika mapigano hayo ni kusitishwa kwa mapigano ya aina yoyote.

Hata hivyo, alitaka watu ambao wanahitaji msaada wa kibinadamu, lazima wafikiwe haraka iwezekanavyo.

Guterres aliongeza kuwa sasa ni wakati wa kuanza mazungumzo na maridhiano.

Ofisi ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa, ilitaka mamlaka nchini Ethiopia kuhakikisha inatoa ulinzi wa raia, ikisema mashambulizi ya kiholelea yanayolenga shabaha zisizo za kijeshi yanaweza kuwa uhalifu wa kivita.

**DW**

# Korea kaskazini yazidi kurusha makombora

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

Korea Kaskazini imerusha makombora mawili kutoka kwenye reli, hili likiwa jaribio la tatu la silaha ndani ya mwezi huu licha ya vikwazo vipya vya Marekani.

Jaribio hilo la makombora liliripotiwa jana na shirika la habari la serikali ya nchi hiyo (KCNA).

Jeshi la Korea Kusini limesema kuwa liligundua kurushwa kwa makombora mawili ya masafa mafupi siku ya Ijumaa nyakati za alasiri, saa chache baada ya Korea Kaskazini kuishutumu Marekani kwa kile ilichokiita uchokozi kuhusiana na vikwazo vipya. KCNA iliripoti kuwa maofisa wa Korea Kaskazini, walisema kuwa majaribio hayo yalifanywa kuangalia na kutathmini ustadi katika taratibu za utekelezaji wa kikosi kinachoendeshwa kwa kutumia treni.

Korea Kaskazini ilifanya jaribio la kwanza la kurusha makombora kutoka kwa treni mnamo Septemba 2021.

KCNA ilisema kuwa uzinduzi huo ulionyesha weledi na kasi ya juu ya mashambulizi na kwamba masuala yalijadiliwa kuweka mfumo sahihi wa uendeshaji wa makombora ya reli kote nchini humo.

**DW**

## MAKALA

# VIONGOZI WA SERIKALI HESHIMUNI NA KUZITII SHERIA ZA BARABARANI



Na Magabilo Masambu

**Pamoja na pongezi hizo kuna kazi kubwa inatakiwa kuendelea kufanyika ili kuhakikisha ajali za barabarani hasa ambazo zinatokana na mwendokasi na uzembe haziendelei kugharimu maisha ya Watanzania.**

AWALI ya yote, nitumie fursa hii kulipongeza Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kazi na juhudi kubwa iliyofanywa kwa miaka kadhaa kuhusu kupunguza na kukinga kutotokea kwa ajali nyingi katika barabara zetu, ambazo awali ziliteketeza sana ndugu zetu. Yote hiyo ni kutokana na mwendokasi wa vyombo vya moto barabarani.

Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Wakati wa Mzee wa Nyakuanyakua, Fortunatus Musilimu, kama msimamizi mkuu wa usalama barabarani, yeye na wenzake walifanya kazi nzuri ya kusaidia kuwadhibiti madereva wasioheshimu sheria za barabarani. Naamini hata wa sasa anafanya kazi nzuri ambayo inatakiwa kuendelea kukaziwa zaidi.

Pamoja na pongezi hizo kuna kazi kubwa inatakiwa kuendelea kufanyika ili kuhakikisha ajali za barabarani hasa ambazo zinatokana na mwendokasi na uzembe haziendelei kugharimu maisha ya Watanzania. Hii ni kwa sababu wanasema kwenye msafara wa mamba kenge huwa hawakosekani.

Katika kuwepo kenge hao, suala la rushwa kwa baadhi ya askari wetu bado lipo na inavyoonekana linataka kuwa kubwa kuliko miaka mitano iliyopita. Kwa maoni yangu, ni jambo linalotakiwa kudhibitiwa vilivyo, vinginevyo tutarudi miaka karibu 15 nyuma na ajali zitaongezeka.

Tukiachana na suala la uzembe na rushwa za barabarani, kuna suala la baadhi ya viongozi wa serikali kujiona wako juu ya sheria za barabarani na kwamba sheria hizo wao haziwahusu. Wanaona kama vile sheria hizo wametungiwa watu wengine na wao hawastahii kuzitii.

Ni jambo la kawaida sana kwa baadhi ya viongozi wa serikali kuendeshwa kwa mwendo mkali zaidi barabarani bila kuheshimu sheria. Mara zote viongozi hao wamekuwa hawasimamishwi wanapovunja sheria. Nadhani si utamaduni mzuri kiongozi wa serikali kutoheshimu sheria za barabarani kwa visingizio vya kuwahi vikao na mikutano jambo ambalo linahatarisha maisha yao.

Sheria zozote zinapotungwa lengo lake ni kuzuia au kukinga madhara fulani kutokea. Bendera tunazokuwa nazo kwenye magari, bahati mbaya sana huwa hazizuii ajali na madhara yake kutokea. Wakati mwingine tunazitumia vibaya kwa kutofuata sheria za barabarani kwa sababu tu tunadhani tunayo kinga ya kutoshtakiwa tunapovunja sheria.

Ninakubali kwamba si ajali zote zinazotokea husababishwa na mwendokasi wa vyombo vya moto. Lakini kama mwendokasi ni sababu mojawapo ya kutokea kwa ajali, kwa nini tusiamini kwamba inaweza kuwa sababu ya vifo vingi barabarani? Wakati mwingine tunawapa wakati mgumu askari wa barabarani namna ya kuwaeleza kupunguza mwendo tuwapo barabarani.

Askari wengi wanaona kabisa kwamba kwa mwendo huu, hawa watu wanaweza kupata ajali lakini kwa sababu wanalinda ugali wao, hawawezi kuthubutu kuwaambia viongozi kwamba mnazidisha mwendo. Badala yake wanaamua kunyamaza litakalotokea litokee.

Viongozi tunapaswa kuwa mfano katika kulinda na kuheshimu sheria zetu na si za barabarani pekee bali hata sheria zingine ambazo tunataka wananchi watekeleze. Mfano unaweza kushangaa askari aliyepakizwa kwenye bodaboda bila kuvaa kofia ngumu kichwani, kumkamata bodaboda aliyempakiza abiria asiye na kofia hiyo! Wakati mwingine tukishindwa kuzitii sheria zetu wenyewe na tukataka ziheshimiwe na wengine. Tutakuwa tumefanya jambo la uonevu mkubwa, hivyo tuanze sisi ili raia wajifunze kwa kuona na kila mtu atatii sheria bila shuruti.

Kifo huwa kinatenda haki tu. Chenyewe hakijui kama wewe ni mkuu wa mkoa, wilaya, polisi, mkurugenzi, katibu tawala, mwalimu, mwandishi wa habari na kadhalika. Wala hakifahamu kama unawahi kikao au la. Ikitokea tu unakiuka sheria barabarani kinafanya kazi yake. Hivyo ni wajibu sisi sote bila kujali tuna mamlaka au la kutii sheria barabarani bila shuruti, hapo tutakuwa tunaziokoa nafsi zetu wenyewe na umauti.

Mara nyingi tunawaona askari barabarani wakiwa na tochi za kusoma mwendokasi wa magari. Sina hakika kama wameziseti kiasi ambacho haziwezi kusoma mwendo mkali wa magari ya viongozi wa serikali na kwamba ile tabia ya askari ya kusoma spidi halafu anatuma picha kwa askari aliyeko mbele haiwahusu viongozi. Kama kamera hizo zinasoma mwendokasi kwa nini viongozi huwa hawasimamishwi na kuonywa kwa mwendo mkali ambao unaweza kugharibu maisha yao? Ni kweli wanakuwa wanawahi vikao lakini ajali huwa hazijui.

Tumejikuta tumejenga utamaduni wa viongozi mahali pengine kutotii sheria, hata kwa mambo yanayohusu maisha yao. Jambo hili ni hatari sana. Kiongozi anavunja sheria halafu anayeomba msamaha ni anayetakiwa kusimamia sheria hizo. Uliona wapi?

Ushauri wangu, kwa sababu suala la ajali barabarani halitazami nafasi ya mtu ana cheo gani, ni mkubwa kiasi gani, basi tutii sheria kama ambavyo tunataka raia azitii sheria hizo. Tutakuwa tumewasaidia sana askari wetu kutokuwa na msongo wa mawazo pale ajali za viongozi zinapotokea wakati tochi zimepigwa na kuonekana hatua hazikuchukuliwa mapema.

Tujipende na tuupende uhai wetu ili tuwe na nafasi zaidi ya kulitumikia taifa letu tukiwa wazima wenye afya tele. Mungu ibariki Tanzania.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kisa cha Cleopatra kilivyosimuliwa na Zahir Ally



Na Adam Fungamwango

INASEMEKANA kuwa hakuna kitu chochote duniani kizuri au kibaya kinachofanyika sasa ambacho hakikufanyika miaka ya nyuma. Kama ni watu wema walikuwapo zamani na watu wabaya zaidi kuwahi kutokea walikuwapo pia zamani. Vyote vinavyotokea kwenye karne hizi ni marudio tu.

Tunaposoma hata vitabu kwa Mungu, tunakutana na habari hizo za kuwapo watu waliokuwa wema kwa binadamu wenzao. Pia hata wafalme wakatili kupita kiasi, hadi sasa ikalazimu Mwenyezi Mungu mwenyewe kuingilia kati na kuwaadhibu kwa mkono wake, maana ya binadamu ilishindikana.

Hata kwenye masuala ya urembo, inasemekama mpaka sasa hakuna mwanamke yeyote mrembo kwenye dunia hii aliyewahi kumshinda mtawala wa Misri, Cleopatra.

Hebu fikiria, warembo hawa wote unaowaona, lakini hadi leo hakuna yeyote anayebisha kuwa Cleopatra, ndiye alikuwa mrembo bora zaidi kuwahi kutokea duniani! Hata wale wabishi, kama vile wanasanyansi na wachunguzi wengine wameshindwa kukana, badala yake wanakubaliana na hilo.

Ameandikwa katika vitabu na majarida mengi na inasemekana kuwa mbali na urembo, na kazi yake ya kutawala, alikuwa pia na akili, busara, akiongozwa pia na Mwenyezi Mungu. Alikuwa akiomba na kusoma vitabu vya Mungu anapokwenda kutatua migogoro na matatizo kadhaa na alifanikiwa licha ya kwamba alikuwa akikabiliana na nguvu za wachawi wakubwa waliokuwapo nchini Misri.

Kama utasoma kisa cha Musa na Firauni, basi utakubali kuwa Misri ilikuwa na wachawi waliokubuhu, waliotaka kushindana hata na Mungu, lakini baadaye akawaangamiza.

Mwanamuziki Zahir Ally Zorro naye hakuwa nyuma, akisimulia kisa cha Cleopatra kwenye wimbo wake alioutoa mwanzoni mwa miaka ya 1990, akiwa na bendi ya Sambulumaa. Aliuita 'Cleopatra.'

"Ulimwengu unayo taarifa hiyo sahihi ee, na kila mwana historia, anakubaliana nayo hiyo, kwamba. Tokea alipoishi chini ya anga la nchi ya Misri, Cleopatra malkia, ulimwenguni inasemakana, hajazaliwa tena, mwanamke yoyote awe na sifa ya urembo kama wa kwake yeye. Cleopatra alikuwa mtawala wa nchi ya Misri, kipindi kirefu nyuma, kabla hajazaliwa Masiya, Bwana Yesu Kristo.

"Alijaliwa urembo kupindukia, alivaa nguo za hariri akijipamba kwa mikufu ya dhahabu na vito vya almasi pamoja na yakuti na marijani. Sauti yake kila alipozungumza, ilishinda nguvu za wachawi na nguvu za washirikina, waliotapakaa kwa wingi enzi zile katika nchi ya Misri. Wamisri walipatwa na wazimu, siku alipokufa Cleopatra, wengi walikufa naye siku hiyo alipogongwa na nyoka kobra."

Hayo ni maneno yaliyomo kwenye wimbo huo. Zahir Ally hakuacha kitu. Alimpa sifa zake za uzuri, urembo na jinsi alivyokuwa akivaa na kujipamba. Lakini alimpa sifa yake kuwa sauti yake kila alipozungumza ilishinda nguvu za wachawi na washirikina waliotapakaa nchini humo.

Kama nilivyosema, Cleopatra alitumia baadhi ya aya za Vitabu Vitakatifu kusoma na kumwomba Mungu kabla hajaenda kuamua kesi na migogoro na mambo mengine ya kiutawala na alifanikiwa, licha ya ushindani mkali kutoka kwa wachawi na watu wabaya kama walivyomfanya Musa. Aliwashinda kutokana na kuwa ni mtu wa Mungu.

Pia tunaona hata kifo cha Cleopatra kilivyotokea kwa kugongwa na nyoka, aina ya kobra. Kifo chake kilishtua wananchi wengi, wengine wakachanganyikiwa na kufa kwa sababu mbalimbali za mihemko, kama kujiua, kufa kwa mshtuko na kujirusha kwenye majengo. Hii ilidhihirisha jinsi alivyopendwa. Nadhani kuna wengine walichanganyikiwa, kwa kuona inakuwaje mwanamke mzuri kama yule anakufa.

Zahir Ally alikisimulia kisa hiki kama picha ya Kihindi. Picha inaweza kuanza mwisho, au katikati, halafu baadaye ndiyo inaanza mwanzo, kutegemeana na jinsi wenyewe walivyotaka iwe.

Naye alifanya hivyo kwa sababu huku kwenye maneno ya mwisho, ndiko kulikuwa na msingi wa wimbo wenyewe. Na ndiko kulitakiwa kuwe mwanzo.

Alikwenda Mwanza na bendi ya Sambulumaa, akakutana na msichana mmoja mrembo, akamuuliza jina, msichana akajibu naitwa Mariam Cleopatra. Alikuwa msichana mzuri kiasi cha urembo wa jina hilo. Lilimfanya Zahir Ally aanze kumkumbuka Cleopatra wa Misri. Ndipo akaanzia wimbo kwenye kumkumbuka mrembo huyo wa Misri, halafu mwisho wa wimbo, ndipo kuna mwanzo na kisa chenyewe.

"Kisa huandamana na tenzi. tulikuwa tuko Mwanza mama, na Sambuluma, safari inaongozwa na Viking (Nguza). Macho yangu yanaona nyota duniani, yamependeza sana, jina lako nani niambie, naitwa Mariam Cleopatra. Bahati mbaya nilioa zamani ningefunga ndoa na yeye, mapenzi yananivunja mgongo..."

Hiki ndicho kisa cha Cleopatra wa Misri, kilichokumbukwa na Zahir, baada ya kukutana na Mariam Cleopatra Kanda ya Ziwa, Mwanza.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya Siri-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MWAHIJA alishusha pumzi kwa nguvu na kutulia tuli. Kwa uzoefu wa Eddy ilimpa picha kuwa tayari ameshamaliza kazi hiyo. Wala hakuwa na haja ya kumuuliza kama amekubali au la.

Kwa muda mrefu hakuwa na mpenzi yoyote. Na hii ilitokana na kukabiliwa na kazi nyingi ambazo zilimfanya kuhamahama huku na huko kiasi cha kumfanya asitulie na kutafuta mwanamke mmoja akatulia naye.

Hata hivyo, ndani ya nafsi yake, alitokea kumpenda Mwahija siku ya kwanza tu alipomuona. Hakutaka kumpoteza hata chembe licha ya kwamba alikwenda pale kikazi. Ni msichana aliyekidhi vigezo vyote anavyohitaji, ikiwamo moyo wake kusuuzika kila anapomwona. Siku zote moyo ukipenda, hakuna kiungo chochote cha mwili kinachoweza kuuzuia.

"Tunaenda nyumbani kwangu leo?"

"Leo hapana, sijaaga kuwa nakwenda kulala sehemu. Si nilikwambia kuwa naishi kwa mama mdogo?"

"Okay nimekuelewa, tukitoka hapa nakurudisha hadi nyumbani, halafu baada ya siku chache jiandae nije kwa mama yako mdogo." Ni kama Mwahija alishtuka hivi. "Uje kwetu?"

"Ndiyo, nakuja ili mama yako mdogo anione, au hutaki anione mama yako?"

"Hapana, nilikuwa siamini kama kweli unaweza kuja nyumbani kwetu na kukutana na mlezi wangu."

"Ndiyo nakuja kwanza, ili hata siku akiona umechelewa, aniulize mimi kuwa huyu mtu yuko wapi." Mwahija hakusema kitu, bali tabasamu pana, lililomnyong'onyesha Eddy. Akamkumbatia na kumbusu.

******************************

Zamani lilikuwa eneo ambalo lilikuwa mbali na nje kabisa ya jiji la Dar es Salaam. Lakini kwa sasa tayari kuna wakazi wengi sana. Ni moja kati ya maeneo yanayokua kwa kasi sana

Wakati huo ukimwambia mtu kuwa nakwenda Goba, anakuangalia mara mbili mbili. Kwa asilimia kubwa lilikuwa pori na mbali sana kwa sababu hata kufikika ilikuwa taabu sana kutokana na kutokuwa na barabara ya uhakika. Waliishi watu wachache sana na waliokuwa wakienda, mara nyingi ni shambani.

Eddy alifika huko na gari yake bila taabu yoyote.




**"Ahsante sana." Alijibu Eddy. Alikaribishwa kwenye kigoda. Baada ya kukaa na yeye kukaa kwenye kiti cha marimba, akakohoa tena na kutema makohozi pembeni.**

Ilikuwa wiki moja baada ya kuachana na Mwahija kwenye baa ya Fabrice.

Ilikuwa siku ya furaha kubwa sana kwake kuonana na kuongea na mwanamke ambaye ghafla tu, ametokea kumpenda.

Mfamasia ambaye alikwenda pale, baada ya mwanamke huyo kwenda kutoa ushahidi wa msichana Tina kununua dawa kwenye duka lake, ambazo baadaye zinageuka sumu na kumuua mfanyabiashara Hafidh Chilambo.

Alikwenda pale kikazi. Lakini kazi sasa imezaa penzi. Pamoja na kuanza penzi zito na msichana huyo, Eddy bado hakukiuka kitu chochote kile kwenye upelelezi wake. Kwanza kabisa ni kwamba bado hajamtajia jina lake halisi. Hadi sasa kwa mpenzi wake anatambulika kwa jina la Danny. Anatambulika kwa Mwahija kama ni mjomba wa Tina, msichana aliyehukumiwa kunyongwa baada ya ushahidi kuonyesha kuwa alimuua Chilambo.

Na mpenzi wake mpya, hajajua kama mpenzi wake yuko kwenye harakati za kumsaka mtu aliye nyuma ya pazia ya kifo cha Chilambo kwani hakuamini kabisa kuwa msichana wa miaka 18, dada wa kazi za ndani, anaweza kufanya jambo lile bila msaada wowote ule. Nia ni mtu au watu walio nyuma ya mpango huo nao washughulikiwe.

Alishuka kwenye gari lake na kuulizia vijana fulani ambao aliwakuta wako kijiweni. Aliwauliza alipokuwa anataka kwenda. Wakamwelekeza.

Alifika kwenye eneo ambalo lilionekana kabisa kuwa zamani lilikuwa shamba. Ni eneo kubwa la wazi, lakini katikati kulijengwa nyumba ya vyumba viwili tu.

Ni sehemu ambayo alifika kwa miguu kwa sababu gari yake isingeweza kufika. Gari aliiacha mbali kidogo.

"Karibu." Alikaribishwa na mama mmoja ambaye licha ya kumkaribisha kwa bashasha, alikuwa akimshangaa kwa sababu hakuwahi kutembelewa na mgeni wa aina ile pale hata siku moja.

"Ahsante." Alijibu na baada ya kujitambulisha kwa uongo na kweli, alimuuliza mwenyeji aliyekuwa anamhitaji.

"Mzee Kalango, yupo, ngoja nikuitie." Mama huyo alisema huku akisitasita kutokana na kuwa na wasiwasi kidogo na mgeni huyo. Akaingia ndani. Baada ya dakika moja na nusu, akatoka mzee mmoja aliyeonekana ana kati ya miaka 65 na 70.

Mzee huyo mrefu mwembamba, alionekana kudhoofu na hii ilionekana kutokana na uduni wa maisha zaidi na si umri. Alimtazama mgeni wake kwa macho yaliyochoka na mshangao.

"Karibu." Alisema huku akihohoa.

"Ahsante sana." Alijibu Eddy. Alikaribishwa kwenye kigoda. Baada ya kukaa na yeye kukaa kwenye kiti cha marimba, akakohoa tena na kutema makohozi pembeni.

"Unasemaje kijana, ulikuwa unahitaji kiwanja?" Ilikuwa ni sauti za mzee Kalango.

"Kwani mzee wewe ni dalali?"

"Ndiyo, kwani wewe umeambiwaje ulivyokuja?"

Ilibidi Eddy abadilishe hadithi na kujitambulisha kuwa hajafika pale kufuata mashamba, ila ni askari polisi aliyekuja kumuuliza maswali kadhaa yanayohusu maisha ya marehemu Hafidh Chilambo, ikiwamo siku ya tukio ambayo aliuawa. Eddy alitoa kitambulisho cha uongo.

"Ni kwamba Tina amehukumiwa kunyongwa, lakini kuna watu bado wanatafutwa wafunguliwe mashtaka. Wewe ulikuwa mlinzi kwenye nyumba hiyo. Na taarifa nilizozipata kuwa uliacha au kuachishwa kazi wiki moja baada ya tukio hilo. Sina ugomvi na wewe mzee na wala serikali haina matatizo na wewe. Jibu ambalo nitakalokuuliza na ambalo unalifahamu tu basi. La sivyo na wewe utafunguliwa mashtaka."

Mshangao na woga mkubwa ulimpata mzee Kalango. Alionekana kutetemeka.

"Usiogope mzee, sema tu unayoyajua na kujibu maswali yangu kwa ufasaha, basi."

"Sawa kijana nitajibu yote." Alijibu kwa hofu.

Mwahija ndiye aliyeifanya kazi ya kumfahamisha na kumwelekeza mzee Kalango anakoishi. Eddy, pamoja na mapenzi, alianza kumtumia msichana huyo kwenye mambo yake ya kipelelezi bila yeye kujijua.

Alichoambiwa ni kujua mlinzi wa zamani kwenye nyumba huyo yuko wapi. Aliambiwa kuwa huyo ndiye anayejua Tina alifanya kazi miaka mingapi na akimpata hawezi kumwongopea, tofauti na mke wa marehemu na ndugu wengine.

Mwahija alidanganywa na Eddy kuwa anachotaka kupata stahiki zote za Tina, ili akampoze mama yake kijijini na yeye akakubali kuifanya kazi hiyo bila kujua.

Mfamasia huyo ambaye ofisi yake ya duka la dawa haiko mbali sana na nyumba hiyo, aliteta na kuongea na majirani, hatimaye mmoja akamwambia kuwa anaitwa mzee Kalango, alikutana naye Goba. Na akamwelekeza sehemu anayoishi. Eddy alipewa taarifa na ramani na mpenzi wake, hiyo ndiyo aliyotumia kufika pale.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# TANTINE KUWAKUTANISHA NA 'BWANA NDIYE MCHUNGAJI'

MWIMBAJI anayekuja kwa kasi kwenye muziki wa injili, Tantine Esther, amewaomba mashabiki wake kuipokea video ya wimbo wake mpya, 'Bwana Ndiye Mchungaji'.

Akizungumza na Nipashe jana, Tantine alisema anamshukuru Mungu kwa mapokezi ya wimbo huo kwa njia ya audio yamekuwa makubwa, hivyo anategemea hali itaongezeka kupitia video hiyo.

"Nimefungua mwaka na wimbo huo ambao umefanyika baraka kwa wengi, video imetoka Ijumaa na tayari ipo kwenye chaneli yangu ya YouTube hivyo naomba zaidi kuniunga mkono ili tuzidi kumtukuza Mungu pamoja," alisema Tantine.



# TID

## AKEMEA NYIMBO ZA NGONO

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, TID, ameamua kulifunua kombe kwa kusema wasanii wa sasa wametawaliwa na mawazo ya ngono kiasi nyimbo zao nyingi zina chembechembe za udhalilishaji.

TID, amesema nyimbo za wasanii wengi zina maana sawa hasa katika zuala la mapenzi, kiasi ambacho inafikia wakati huwezi kusikiliza kutokana na maneno ya kuwadhalilisha wanawake.

"Watu wamekua wakichochea ngono na kudhalilisha wanawake, sidhani kama tutaachia urithi mzuri vijana wetu". Amesema TID.

# Mwijaku kiti cha moto hichoo, utakiweza?

KITENDO cha mwigizaji na staa wa mitandao ya kijamii, Mwijaku, kuchukua fomu ya kuwania nafasi ya uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimeibua mjadala mkali wenye mitazamo tofauti.

Mara alipochukua fomu hivi karibuni katika Ofisi ndogo za Makao Makuu ya CCM, jijini Dar es Salaam, baadhi ya wasanii wamejitokeza na kueleza Mwijaku, amefanya hivyo kwa nia ya kupata umaarufu baada ya kuona anaporomoka kwa kasi.

Mrisho Mpoto, amesema hakubaliani na Mwijaku kuchukua fomu hiyo, kwani jinsi alivyo si mahali pake na angekaa ili kuwapisha watu wenye uwezo kuwania.

Hata hivyo, Mwijaku amesema anajiona ana uwezo wa kushika nafasi hiyo, kamwe hawezi kuvunjika moyo na watu wenye husda kwake.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE, PSG WATETA
KYLIAN Mbappe mwenye umri wa miaka 23 anajadiliana na Paris St-Germain kuhusu mkataba mpya. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa alitarajiwa kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake utakapokamilika mwishoni wa msimu huu. ***(Telegraph)***

### HAALAND SASA AFUNGUKA
ERLING Braut Haaland amesema Borussia Dortmund inamshinikiza kufanya uamuzi kuhusu hatima yake. Klabu kadhaa za Ulaya zimehusishwa na uhamisho wa mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Norway. ***(Guardian)***

### VLAHOVIC KUTUA ARSENAL
KLABU ya Fiorentina inakaribia kukubali dau la pauni milioni 58 kutoka Arsenal kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji huyo matata wa Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. ***(La Repubblica)***

### BARCA, BAYERN VITANI
KLABU za Bayern Munich na Barcelona zinataka kumsajili beki wa Chelsea na Denmark, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 25, wakati mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### CONTE ATOA MSIMAMO
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte ambaye mkataba wake wa sasa unaendelea hadi mwisho wa msimu ujao, amekataa kutoa hakikisho kuhusu hatima yake ya baadaye na kusema kuwa anazingatia jukumu lake la sasa. ***(Guardian)***

### NDOMBELE MAMBO MAGUMU
KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 25 anafanya mazoezi mwenyewe huku hatima yake ya baadaye katika klabu ya Spurs ikiwa mashakani. ***(Football London)***

### INZAGHI KUTUA UNITED
KLABU ya Manchester United imewasiliana na kocha wa Inter Milan, Simone Inzaghi kuhusu uwezekano wa kujiunga nao msimu huu wa joto, huku Mtaliano huyo akikaribia kuanza masomo ya lugha ya Kiingereza. ***(Corriere Dello Sport)***

### HENDERSON SOKONI
KLABU ya Southampton imeulizia kuhusu usajili wa mlinda mlango wa Manchester United mwenye umri wa miaka 24, Dean Henderson kwa ajili ya dirisha hili la Januari. ***(Football Insider)***

### BROJA KITAELEWEKA EPL
SOUTHAMPTON ina nia ya kubadilisha mkopo wa Armando Broja kutoka Chelsea kuwa mkataba wa kudumu, ingawa huenda wakakabiliwa na ushindani wa kumnunua mshambuliaji huyo wa Albania mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Sports)***

### MELO SAFI ARSENAL
ARSENAL wamepiga hatua katika mazungumzo yao na Juventus kuhusu usajili wa mkopo wa miezi sita wa kiungo wa kati mwenye umri wa miaka 25, Arthur Melo. ***(Telegraph)***

### BLAS ANUKIA ENGLAND
KLABU za Newcastle United na Watford zinavutiwa na winga wa Nantes, Ludovic Blas mwenye umri wa miaka 24. ***(Star)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MODRIC AKUBALI KUBAKIA MADRID

●●●Uamuzi huo wa kuongeza mkataba mpya utamaliza tetesi kuwa ...

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Real Madrid, Luka Modric ataongezwa mkataba mpya wa mwaka mmoja ili kuendelea kubakia kwa miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa mujibu wa ESPN.

Ripoti hiyo imebainisha Real Madrid bado haijapata mbadala wa kiungo huyo raia wa Croatia, hivyo uamuzi wa kumpa mkataba mwingine wa kuitumikia klabu hiyo ili abakie hapo hadi mwakani.

Akiwa bado anatumikia mkataba wa miezi 12 ambao bado haujatamatika, kulikuwa na uvumi kuna uwezekano Modric akaondoka hapo Santiago Bernabeu baada ya msimu huu kumalizika.

Lakini sasa ripoti hiyo imebainisha nyota huyo mshindi wa pili wa Kombe la Dunia mwaka 2018 ataendelea kukipiga kwenye klabu hiyo.

Kwa hali ilivyo, uwezekano wa Modric kuongeza mkataba wa mwaka mmoja zaidi ni mkubwa.

Hii ni baada ya mchezaji huyo kukubali vipengele vya mkataba mpya na sasa, ni suala la muda tu kabla ya pande zote zinazohusika na mchakato huo kukamilisha zoezi hilo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Hispania, Real Madrid iko kileleni ikiwa na pointi 49 ikifuatiwa na Sevilla yenye pointi 44 wakati Barcelona ambayo bado inaendelea kusuasua iko katika nafasi ya sita ikiwa na pointi 32.

Levante yenye pointi 11 ndio inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo ya juu Hispania inayoshirikisha timu 20.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
TOTTENHAM
VERSUS
ARSENAL
1 | 2.38
X | 3.31
2 | 2.96

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BENITEZ: KUUZWA DIGNE ILIKUWA BIASHARA NZURI

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Everton, Rafael Benitez amesisitiza kuondoka kwa Lucas Digne ni biashara nzuri kwa klabu yake.

Mlinzi huyo wa kushoto kutokea taifa la Ufaransa amejiunga na klabu ya Aston Villa kwa uhamisho uliogharimu kiasi cha pauni milioni 25 baada ya kupoteza matumaini akiwa chini ya Benitez kwenye viunga vya Goodison Park.

Benitez alinukuliwa akisema, "ni jambo zuri, kumbadilisha mchezaji ambaye alikuwa anafikisha miaka 29 na wachezaji vijana, mimi ni kocha na nawajibika na maamuzi yangu, ni muda wa kuifikiria timu na mipango ya baadaye, inabidi tusonge mbele."

Digne ambaye amesaini mkataba wa miaka minne na nusu na Aston Villa alisema hakutarajia kuondoka kama alivyoondoka kwenye viunga vya Goodison Park huku akimtuhumu kocha wake. "Ni mtu mmoja wa kutoka nje ambaye ataharibu mapenzi yako" alichapisha kwenye ukurasa wake wa Instagram.

# Barca kumtoa mkopo Depay



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Klabu ya Barcelona, Xavi yupo kwenye mikakati ya kumpeleka kwa mkopo nyota wa timu hiyo, Memphis Depay, kwa mujibu wa Marca.

Mkopo huo ni wa miezi sita na sababu kubwa ili kumsaidia nyota huyo kupata nafasi ya kucheza na raia mwenzake wa Uholanzi, Luuk de Jong.

Mshambuliaji Depay amekuwa na msimu mzuri ndani ya Barcelona huku akifunga mara nane kwenye michezo 16 ya LaLiga.

Lakini hajaweza kumshawishi kocha wake huyo aliyetua Novemba, mwaka jana akichukua mikoba ya Ronald Koeman.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Xavi amekuwa akivutiwa zaidi na de Jong, huku wiki za karibuni amekuwa akimtumia zaidi na kufunga katika mechi tatu zilizopita.

Katika mchezo wa El Clasico, Depay alianzia benchi huku De Jong akiwa kwenye kikosi cha kwanza, wakati mchezo wake wa kwanza dhidi ya Mallorca mwaka huu 2022 aliweza kufunga huku siku sita baadaye akifunga tena dhidi ya Granada.

Xavi kwa sasa yupo kwenye harakati za kukiimarisha kikosi chake hicho ambacho kimekuwa na mwanzo mbaya wa msimu huu wa Ligi Kuu Hispania.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 16/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3175 | Altay vs Alanyaspor | 2.45 | 3.36 | 2.71 |
| 14:00 | 1632 | Nacional Madeira vs Benfica Lisbon B | 2.09 | 3.37 | 3.22 |
| 14:00 | 2152 | Atletico Baleares vs Valencia | 4.64 | 3.85 | 1.67 |
| 14:15 | 2825 | Utrecht vs Ajax | 5.89 | 4.81 | 1.42 |
| 14:30 | 1527 | Sassuolo vs Verona | 2.21 | 3.65 | 3.00 |
| 15:00 | 3093 | Hull City vs Stoke City | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 15:00 | 4089 | Rennes vs Bordeaux | 1.42 | 4.88 | 6.37 |
| 15:30 | 1325 | Sandhausen vs Jahn Regensburg | 2.86 | 3.35 | 2.32 |
| 15:30 | 3846 | Royal Antwerp vs Charleroi | 2.00 | 3.64 | 3.34 |
| 15:30 | 4457 | Schalke 04 vs Holstein Kiel | 1.85 | 3.58 | 3.83 |
| 15:30 | 5687 | Heidenheim vs Ingolstadt | 1.66 | 3.69 | 4.82 |
| 16:00 | 1481 | Gambia vs Mali | 5.14 | 3.26 | 1.76 |
| 16:00 | 5119 | Giresunspor vs Kasimpasa | 1.96 | 3.35 | 3.75 |
| 16:00 | 5897 | Elche vs Villarreal | 4.31 | 3.71 | 1.79 |
| 16:30 | 2622 | Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.39 | 3.43 | 2.70 |
| 16:30 | 5168 | Groningen vs PSV Eindhoven | 7.47 | 4.91 | 1.35 |
| 17:00 | 1064 | Monaco vs Clermont Foot | 1.48 | 4.46 | 6.14 |
| 17:00 | 1131 | Venezia vs Empoli | 2.69 | 3.49 | 2.48 |
| 17:00 | 3016 | West Ham vs Leeds | 1.63 | 4.18 | 4.78 |
| 17:00 | 3046 | Reims vs Metz | 1.78 | 3.47 | 4.67 |
| 17:00 | 4595 | CD Trofense vs Porto B | 3.12 | 3.32 | 2.16 |
| 17:00 | 4756 | Lorient vs Angers | 2.36 | 3.19 | 3.04 |
| 17:00 | 4966 | Strasbourg vs Montpellier | 2.02 | 3.48 | 3.53 |
| 17:00 | 5324 | Liverpool vs Brentford | 1.30 | 5.40 | 9.41 |
| 17:30 | 3274 | Augsburg vs Eintracht Frankfurt | 3.27 | 3.47 | 2.12 |
| 17:45 | 5416 | AL Akhaa AL Ahli vs Al-Nejmeh | 11.53 | 5.76 | 1.19 |
| 18:00 | 4522 | Eupen vs Cercle Brugge | 3.11 | 3.35 | 2.20 |
| 18:15 | 1989 | AEK Athens vs Panetolikos | 1.30 | 5.11 | 9.24 |
| 18:30 | 5956 | Santa Clara vs Tondela | 1.86 | 3.45 | 4.04 |
| 18:45 | 5845 | Fortuna Sittard vs AZ Alkmaar | 6.28 | 4.81 | 1.40 |
| 19:00 | 3825 | Tunisia vs Mauritania | 1.33 | 4.38 | 10.94 |
| 19:00 | 5050 | Ivory Coast vs Sierra Leone | 1.32 | 4.35 | 11.85 |
| 19:00 | 5842 | Hatayspor vs Galatasaray | 3.06 | 3.40 | 2.20 |
| 19:05 | 2260 | Troyes vs Lyon | 4.08 | 3.73 | 1.81 |
| 19:30 | 2378 | Tottenham vs Arsenal | 2.38 | 3.31 | 2.96 |
| 19:30 | 2420 | Arminia Bielefeld vs Greuther Furth | 1.95 | 3.44 | 3.84 |
| 20:00 | 1479 | Apollon Limassol vs Omonia Nicosia | 2.14 | 3.32 | 3.32 |
| 20:00 | 5322 | Roma vs Cagliari | 1.38 | 5.00 | 7.40 |
| 20:30 | 3062 | PAS Giannina vs Atromitos | 1.94 | 3.21 | 4.05 |
| 20:30 | 4790 | Panathinaikos vs Olympiakos | 4.14 | 3.25 | 1.90 |
| 20:30 | 4990 | Anderlecht vs Standard Liege | 1.45 | 4.63 | 5.91 |
| 21:00 | 2847 | Deportivo Toluca vs Santos Laguna | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 21:00 | 5231 | Ironi Kiryat Shmona vs Beitar Jerusalem | 2.29 | 3.09 | 2.94 |
| 21:00 | 5512 | FC Vizela vs Sporting Lisbon | 9.86 | 5.33 | 1.27 |
| 21:30 | 1956 | Famalicao vs Pacos Ferreira | 2.02 | 3.30 | 3.60 |
| 22:00 | 3310 | Algeria vs Equatorial Guinea | 1.32 | 4.48 | 10.95 |
| 22:45 | 2811 | Marseille vs Lille | 2.32 | 3.28 | 3.04 |
| 22:45 | 4101 | Atalanta vs Inter | 2.85 | 3.66 | 2.29 |
| 23:00 | 1291 | Racing Genk vs Kfco Wilrijk | 1.31 | 5.34 | 7.90 |
| 23:30 | 1073 | Belenenses vs Porto | 14.81 | 6.71 | 1.16 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KOCHA AZAM AKARIBIA KUTUA BIASHARA UNITED

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Biashara United umesema uko katika hatua za mwisho kwenye mchakato wa kumtambulisha aliyekuwa Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati kuchukua mikoba iliyoachwa na Mkenya Patrick Odhiambo, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Biashara United , Selemani Mataso, alisema Vivier amesharejea nchini na yuko mkoani Mara kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo na mabosi wa timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

Mataso alisema mazungumzo na Mrundi huyo yanaendelea vizuri na anaamini pande hizo mbili zitaelewana na kufikia hatua ya kumtambulisha rasmi.

"Ni kweli Vivier Bahati yuko hapa Musoma na mazungumzo naye yanaenda vizuri, tunatarajia muda wowote kuanzia leo (jana), tutamtambulisha rasmi baada ya kukamilisha masuala ya kusaini mkataba na taratibu nyingine zinazotakiwa," alisema Mataso.

Aliongeza anaamini kocha huyo ataisaidia timu yao kufikia malengo kwa sababu walianza kumfuatilia kwa muda mrefu na ana faida ya kulifahamu vizuri soka na wachezaji wa Tanzania.

"Ni kocha ambaye anaijua vyema ligi, wachezaji wetu wa Tanzania na Afrika kwa ujumla, hali hii inatupa matumaini kuwa ni mwalimu atakayetusaidia kufikia malengo," Mataso alisema.

Naye kocha huyo alikiri kurejea nchini na kuongeza mazungumzo yake na mabosi wa Biashara United yanaenda vyema.

"Bado sijasaini mkataba, tunaendelea na mazungumzo lakini yako katika hatua nzuri, yakienda sawa sawa basi kila kitu kitawekwa wazi ikiwamo kuanza kazi rasmi ya kukinoa kikosi cha Biashara United," alisema kocha huyo.



Beki wa Ruvu Shooting, Jafari Mbena (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya Rifat Said wa Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mabatini Mlandizi, Pwani juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Shime asifia Tanzanite imeimarika

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), Bakari Shime, amesema ana matarajio kikosi chake kitapata matokeo mazuri katika mechi yao ya raundi ya nne dhidi ya Ethiopia.

Tanzanite Queens itaikaribisha Ethiopia katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia itakayochezwa Januari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Shime aliliambia gazeti hili wachezaji wake wanaendelea vyema na maandalizi na anafurahi kuona wanaimarika na wako tayari kuwakabili Ethiopia.

"Tunajua mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa, kikubwa nimeendelea kuyafanyia kazi mapungufu yaliyokuwapo ikiwamo safu ya ushambuliaji kuongeza umakini ili watumie vizuri nafasi wanazotengeneza," Shime alisema.

Alisema hataki kuona wanaendelea kupoteza nafasi kama ilivyokuwa katika mechi iliyopita dhidi ya Burundi ingawa waliwaondoa majirani hao.

Aliongeza kulingana na ubora wa wachezaji wa Ethiopia, nyota wake wanatakiwa kuongeza utulivu kwa ajili ya kuhakikisha wanapata ushindi mnono hapa nyumbani na kujiweka kwenye nafasi nzuri watakapokwenda kurudiana ugenini.

Michezo
Jumapili Januari 16, 2022
Nipashe



Modric akubali kubakia Madrid

HABARI UK 21

# YANGA YAPANIA KUVUNJA MWIKO

## ●●●Yatamba imeimarika na iko tayari kumaliza 'uteja' Mkwakwani ili...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya misimu sita ya kutopata ushindi dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga, Yanga inashuka dimbani leo kuwavaa wenyeji katika mechi ya raundi ya 12 ya Ligi Kuu Tanzania Bara huku ikidhamiria kuondokana na 'mzimu mbaya' uliowashikilia.

Mara ya mwisho Yanga kupata ushindi kwenye uwanja huo dhidi ya Coastal Union, ilikuwa ni Februari 4, mwaka 2015, na iliwafunga wenyeji bao 1-0, bao la dakika ya 11, shukrani aliyekuwa nahodha na beki mahiri wa kikosi hicho, Nadir Haroub 'Cannavaro'.

Tangu msimu huo wa 2014/15, Yanga kama haitopokea kichapo, basi inaambulia sare kwenye uwanja huo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ambaye amerejea nchini akitokea katika mapumziko mafupi, amesema timu yake ipo tayari kwa mechi hiyo na wamejiandaa kiufundi, mbinu na kiakili kuikabili Coastal Union kwenye mchezo huo ambao ametabiri utakuwa mgumu.

"Timu yangu ipo tayari, kiufundi, kimbinu na kiakili. Nina kila kitu hapa, naijua vizuri Coastal Union, najua wanavyocheza, namjua kocha wao, lakini nawaheshimu. Mpira hauna bla bla kusema lazima tutashinda au tutafanya hivi, hapana, kila kitu kitaonekana uwanjani," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema anafahamu kwa Yanga kila mechi kwao ni ngumu, hivyo wamejipanga imara kukabiliana na ushindani huo.

"Yanga kila mechi kwake ni ngumu, lakini mechi hii ni kubwa zaidi na ngumu, kama tunataka kutwaa kombe tunatakiwa kila mechi kuwa makini nayo na kuichukulia uzito sawa, siyo mechi nyingine tunakuwa makini sana na mechi nyingine umakini unakuwa mdogo. Hii Coastal Union ni timu kubwa ina kocha mzuri na napenda falsafa zake.

"Lakini kwangu mimi na tabia yangu, huwa napenda mechi ngumu kwa sababu napenda kupambana na wachezaji wangu napenda wapambane. Napenda ushindani haijalishi kama utashinda au hutoshinda, lakini ni lazima uwe mpambaji," Nabi alisema.

Kocha huyo raia wa Tunisia alisema anajua wanachama na mashabiki wa Yanga hawana furaha kutokana na matokeo ya kuvuliwa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, lakini hayo yamepita na sasa wanatakiwa wasonge mbele kwa kujipanga na michuano mingine.

Aliongeza matokeo ya msimu uliopita hayawezi yakawapa uhakika wa ushindi Coastal Union, wala Yanga kutokuwa na uhakika wa kuondoka na pointi tatu muhimu.

Wenyeji Coastal Union, pia imebadilika tangu iwe chini ya Kocha Mkuu Mmarekani Melis Medo na ndiyo maana mpaka sasa baada ya miaka mingi, Coastal Union ipo juu kwenye msimamo wa ligi, ikiwa nafasi ya nne kwa pointi 17.

Kocha wa magolikipa wa Coastal Union, Salim Waziri, amesema wamejiandaa vyema kuelekea mechi ya leo, nia na madhumuni ni kuendeleza rekodi yao nzuri na kuifunga Yanga.

"Kwa maandalizi tuko vizuri. Wachezaji wote wako vizuri na wanaitaka hii mechi, kila mmoja ana hamu ili aonyeshe alichokuwa nacho, tunawaambia mashabiki hasa wa Coastal Union wajitokeze kwa wingi kuishangilia timu yao kwa sababu tuna uhakika wa kushinda," alisema kipa huyo wa zamani wa timu hiyo.

Naye Nahodha wa timu hiyo, Mkongomani Paschal Kitenge, alisema wamekaa kambini kwa muda wa wiki mbili kwa ajili ya mechi hiyo.

"Tuko kambini kwa wiki mbili sasa tukifanya mazoezi kwa ajili ya mechi hii. Yanga ni timu kubwa, lakini pia Coastal Union ni timu kubwa, tunazihitaji pointi tatu ili tuwe kwenye nafasi ya tatu, na mimi si mara ya kwanza kucheza dhidi ya Yanga, hivyo sina wasiwasi," alisema.

Msimu uliopita, Yanga ilikanyaga kwenye uwanja huo na kuambulia kipigo cha mabao 2-1, mechi ikichezwa Machi 4, mwaka jana.



Kiungo wa kimataifa wa Yanga, Mukoko Tonombe akiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC, Mbeya City hesabu zimetimia

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikiwasili salama Mbeya, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, amesema ana matarajio makubwa wachezaji wake wataonyesha kiwango bora zaidi katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka jijini Dar es Salaam jana, Pablo alisema ana imani nyota wake wataonyesha ubora mzuri kama walivyofanya katika mechi mbili za mwisho za michuano ya Kombe la Mapinduzi huko Zanzibar.

Pablo alisema wanaenda kucheza na moja ya timu zenye ubora na wamejiandaa kukutana na ushindani huku akiamini wachezaji wake wataonyesha kiwango kizuri na kufuata maelekezo aliyowapa mazoezini.

"Sasa tumerejea katika ligi, ni muhimu zaidi kutafuta matokeo chanya, nina imani zile nguvu tulizotumia katika Kombe la Mapinduzi tutaziweka pia kwenye mechi zetu zijazo ili kuhakikisha tunaondoka na pointi tatu katika kila mechi kwa ajili ya kufikia malengo yetu ya kutetea ubingwa," alisema Pablo.

Aliongeza wachezaji wake wote waliocheza michuano ya Kombe la Mapinduzi wako fiti na wako tayari kupambana ili kuondoka na ushindi dhidi ya Mbeya City.

"Tumefanya maandalizi vizuri, kila mchezaji yuko tayari kwa mechi hiyo, tumetoka katika Kombe la Mapinduzi tukiwa na ari, tumejipanga kuendeleza mazuri kwenye mchezo huo," Pablo alisema.

Kuhusu kiungo, Clatous Chama alisema atakuwa katika msafara wa timu hiyo lakini hatakuwa sehemu ya kikosi kitakachocheza mchezo huo kwa sababu ya kutokuwa 'fiti' kukabiliana na wapinzani.

Wakati huo huo, wachezaji wawili wa kimataifa waliokuja kufanya majaribio kwa mabingwa hao watetezi, Etop David Udoh na Moukoro Cheik Tenena wataondoka nchini leo alfajiri ili kurejea makwao baada ya Pablo kutoridhishwa na viwango vyao.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 9